

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA
MIPANGO KWA MWAKA 2016/17**

Juni, 2016

YALIYOMO

YALIYOMO.....	i
VIFUPISHO VYA MANENO.....	iv
1.0 UTANGULIZI	1
2.0 MWELEKEO KATIKA KUJENGA MSINGI WA UCHUMI IMARA	3
3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2015/16.....	7
3.1 Mapato kwa mwaka 2015/16.....	8
3.2 Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2015/16	8
3.3 Matumizi kwa Miradi ya Maendeleo mwaka 2015/16.....	8
3.4 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2015/16:	9
3.4.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla	9
3.4.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa	9
3.4.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini	10
3.4.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali	11
3.4.5. Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.....	13
3.4.6. Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma.....	14
3.4.7. Usimamizi wa Malipo	16
3.4.8. Deni la Taifa	16
3.4.9. Usimamizi wa Mali ya Serikali	17
3.4.10. Ununuzi wa Umma	17
3.4.11. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.....	20
3.4.12. Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma	22
3.4.13. Mafao ya Wastaifu na Mirathi	23
3.4.14. Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi.....	23
3.4.15. Tume ya Pamoja ya Fedha	24
3.4.16. Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi.....	24
3.5. USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA.....	25
3.5.1. Huduma za Kibenki.....	25
3.5.2. Mifuko ya Hifadhi za Jamii.....	30
3.5.3. Rufani za Kodi.....	32
3.5.4. Huduma za Bima.....	32
3.5.5. Mitaji na Dhamana	33

3.5.6.	Dhamana za Uwekezaji Tanzania	35
3.5.7.	Taasisi za Mafunzo	36
3.5.8.	Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo.....	38
3.5.9.	Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Mwaka 2015/16.....	41
3.6.	MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI	43
3.6.1	MAFANIKIO	43
3.6.2	CHANGAMOTO.....	43
3.6.3	HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO.....	44
4.0	MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17	45
4.1	MAJUKUMU YA WIZARA.....	45
4.1.1	Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla	45
4.1.2	Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa	45
4.1.3	Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini	46
4.1.4	Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali	46
4.1.5	Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.....	47
4.1.6	Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma.....	48
4.1.7	Usimamizi wa Malipo	48
4.1.8	Deni la Taifa	49
4.1.9	Usimamizi wa Mali ya Serikali	49
4.1.10	Ununuzi wa Umma	50
4.1.11	Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.....	51
4.1.12	Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma	51
4.1.13	Mafao ya Wastaafu na Mirathi	51
4.1.14	Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi.....	52
4.1.15	Tume ya Pamoja ya Fedha	52
4.1.16	Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi	52
4.2	USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA.....	53
4.2.1	Huduma za Kibenki.....	53
4.2.2	Mifuko ya Hifadhi za Jamii.....	56
4.2.3	Rufani za Kodi.....	57
4.2.4	Huduma za Bima	57
4.2.5	Mitaji na Dhamana	58

4.2.6	Dhamana za Uwekezaji Tanzania	59
4.2.7	Taasisi za Mafunzo	60
4.2.8	Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo.....	63
5.0	MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2016/17.....	66
5.1	MAKADIRIO YA MAPATO.....	66
5.2	MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17.....	67
5.2.1	FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO	67
5.2.2	FUNGU 21 – HAZINA	67
5.2.3	FUNGU 22- DENI LA TAIFA	68
5.2.4	FUNGU 23 – MHASIBU MKUU WA SERIKALI	68
5.2.5	FUNGU 7 – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA	69
5.2.6	FUNGU 10 – TUME YA PAMOJA YA FEDHA.....	69
5.2.7	FUNGU 13 – KITENGO CHA UDHIBITI WA FEDHA HARAMU	69
5.2.8	FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI	70
5.2.9	FUNGU 66 – TUME YA MIPANGO	70
5.2.10	FUNGU 40 – MFUKO WA MAHAKAMA.....	71
5.2.11	FUNGU 42 – MFUKO WA BUNGE.....	72
5.3	SHUKRANI	72

VIFUPISHO VYA MANENO

CAG	–	Controller and Auditor General
EFDs	–	Electronic Fiscal Devices
EFT	–	Electronic Fund Transfer
HESLB	–	Higher Education Student Loan Board
IFMS	–	Intergrated Financial Management System
IPSAS	–	International Public Sector Accounting Standards
MCA	–	Millenium Challenge Account
MOI	–	Muhimbili Orthopaedic Institute
MSD	–	Medical Stores Department
PEFA	–	Public Expenditure and Financial Accountability
SDL	–	Skills Development Levy
TBC	–	Tanzania Broadcasting Corporation
TEA	–	Tanzania Education Authority
TEHAMA	–	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TFDA	–	Tanzania Food and Drugs Authority
TFNC	–	Tanzania Food and Nutrition Center
TISS	–	Tanzania Inter-Bank Settlement System
TRA	–	Tanzania Revenue Authority
TRL	–	Tanzania Railway Limited
TTA	–	Tanzania Tea Authority
TTCL	–	Tanzania Telecommunication Company Limited
VETA	–	Vocational Education and Training Authority

1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17.
2. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuanza hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17.
3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii adhimu kuwapongeza kwa dhati kabisa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi mkubwa waliopata katika uchaguzi mkuu wa tarehe 25 Oktoba, 2015 na kuwawezesha kuongoza Taifa letu na Serikali ya Awamu ya Tano. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim M. Majaliwa kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kura nyingi kuwa mbunge wao na hivyo kutoa fursa kwa ye ye kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa pamoja, nawaombea afya njema na hekima kutoka kwa Mungu katika kutekeleza majukumu yao chini ya kaulimbiu ya "Hapa Kazi Tu" kwa manufaa ya wananchi wote na hasa masikini.
4. **Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Aidha, nampongeza pia Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kuteuliwa kuwa mbunge na kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na hivyo kukusaidia kuendesha vyema shughuli za Bunge. Nawaombea kwa Mungu awape afya na hekima ya kuendesha Bunge hili kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla.

5. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwakilisha wananchi wa majimbo yenu na wote walioteuliwa kuwakilisha makundi maalum katika jamii yetu. Aidha, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kumsaidia katika kuwaletea maendeleo Watanzania.
6. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniamini na kunateua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hivyo, kwa mara nyingine, ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla kwamba nitatekeleza jukumu hili kwa bidii, weledi na uadilifu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji – Mbunge wa Kondoa, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Nawapongeza pia Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali Dkt. Servacius Beda Likwelile, Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Dorothy S. Mwanyika, Ndugu James Doto na Ndugu Amina Kh. Shaaban kwa kuteuliwa kwao katika nafasi hizo na ninawashukuru kwa kusimamia vyema kazi za kila siku za Wizara yangu. Pia napenda kuwashukuru Prof. Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Bw. Lawrence Mafuru – Msajili wa Hazina na Dkt. Albina Chuwa – Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu vizuri na kuongoza taasisi muhimu wanazosimamia kwa weledi mkubwa. Aidha, nawashukuru Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi nzuri na ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia.
7. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii, kuwashukuru Wenyeviti wa Bunge wote, kwa kuendesha majadiliano ya bajeti kwa mwaka 2016/17 kwa umakini. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Pia, natoa shukrani nyingi kwa Kamati yake kwa ushauri na mapendekezo ambayo yamesaidia sana kuboresha mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa

mwaka 2016/17. Ninaahidi kwa dhati kabisa kwamba tutaendelea kushirikiana na Kamati hii ili kuhakikisha Tanzania inafikia dhamira yake ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

8. ***Mheshimiwa Spika***, hotuba yangu itajikita katika maeneo makuu matatu ambayo ni: Kwanza, ni Mwelekeo wa Majukumu ya Wizara katika Kujenga Msingi wa Uchumi Imara. Pili, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2015/16 na tatu, Malengo na Maombi ya Fedha kwa mwaka 2016/17.

2.0 MWELEKEO KATIKA KUJENGA MSINGI WA UCHUMI IMARA

9. ***Mheshimiwa Spika***, azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuifikisha Tanzania kuwa nchi yenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Ili kufikia azma hii, ni muhimu kuwekeza katika viwanda kama ilivyosisitizwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati akizindua Bunge la 11 tarehe 20 Novemba, 2015.
10. ***Mheshimiwa Spika***, wakati Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb), alipokuwa anawasilisha hotuba yake katika Bunge lako Tukufu mnamo tarehe 25 Aprili, 2016, alielezea mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano yenye falsafa ya HAPA KAZI TU nanukuu **“Malengo ya Serikali ya Kufikia kipato cha kati na kufanyika mapinduzi makubwa ya viwanda yanategemea sana utulivu wa uchumi”, mwisho wa kunukuu.**
11. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu imejipanga kuchukua hatua madhubuti zinazolenga kujenga Taifa linalojitegemea kwa kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Moja ya hatua hizo ni kusimamia na kufuatilia kwa ukamilifu utekekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21. Mpango huu unajikita katika kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu.

12. **Mheshimiwa Spika**, ili mpango huu uweze kutekelezwa kwa ufanisi na kupata matokeo tarajiwa, ni dhahiri kuwa tutahitaji rasilimali za kutosha, hususan rasilimali fedha. Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na wadau wengine inalo jukumu la kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 imeweka bayana majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango ya kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato, kupanua wigo wa vyanzo vipyta vya mapato na kusimamia kwa ufanisi matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali.

13. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato, Wizara itajielekeza katika maeneo yafuatayo:- Kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato; Kurasimisha sekta isiyo rasmi kuingia katika mfumo wa kodi na hivyo kupanua wigo wa kodi na; Kuimarisha ufuutiliaji wa mapato yanayokusanywa na taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Tunalenga pia kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na kuboresha usimamizi wake chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokana na uzoefu na mifumo ya ukusanyaji iliyopo nchi nzima; Kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija; na Kuendelea kuimarisha usimamizi na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara bandarini na maeneo ya mipakani ili kuhakikisha kwamba kodi stahiki zinakusanywa.

14. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, hatua ambazo zitachukuliwa ni pamoja na kuendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato. Napenda kutumia fursa hii kuaagiza kuwa, kuanzia mwaka ujao wa fedha ni lazima mfumo wa kielektroniki utumike katika utoaji wa risiti kwa tozo, faini, ada na malipo mengine yote ya Serikali kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakala wote wa Serikali. Hii itahusisha pia malipo ya faini mahakamani, faini

za usalama barabarani, viingilio kwenye mbuga za wanyama, na vibali vya kuvuna maliasili. Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kusimamia utekelezaji wa agizo hili. Aidha, Serikali imeamua kufanya uthamini wa majengo kwa mkupuo ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo na usimamizi wake kuwa chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanzia mwaka ujao 2016/17.

15. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kutambua mchango mkubwa wa sekta binafsi katika kukuza uchumi. Hivyo, Serikali itatoa fursa kwa sekta hii kushiriki kikamilifu katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ushirikiano na Serikali. Kwa kutambua mchango mkubwa na umuhimu wa sekta binafsi katika kukuza uchumi, Serikali imedhamiria kushughulikia vikwazo mbalimbali kwa ufanyaji biashara na uwekezaji kwa nguvu zaidi.

16. **Mheshimiwa Spika**, Wizara itazingatia sheria, kanuni, taratibu, miongozo na kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Hii ni pamoja na kudhibiti matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima kama vile safari za nje zisizo na tija, sherehe, warsha, semina, ununuzi wa magari na samani. Aidha, Wizara itaimarisha mfumo wa ununuzi wa pamoja wa bidhaa mtambuka Serikalini ili kupata bidhaa bora na thamani halisi ya bidhaa husika.

17. **Mheshimiwa Spika**, Wizara itaimarisha Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kwa kumuongezea wataalam wenye weledi na taaluma mbalimbali ili kumwezesha kupata thamani halisi ya miradi, mifumo na programu mbalimbali za maendeleo. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia jukumu lake la msingi la kufanya kaguzi za ndani ili kuhakikisha kwamba kila taasisi inatumia raslimali za umma kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

18. **Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha uchumi unaendelea kuwa katika hali ya utulivu na kukua kwa kasi, uimara na uwezeshwaji wa sekta ya fedha unahitajika. Hivyo, mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano ni kudhibiti mfumuko wa bei ili uendelee

kubaki kwenye tarakimu moja na hivyo kuzuia kasi ya kupanda kwa gharama za maisha; kudhibiti nakisi ya bajeti ili iendelee kushuka na kufikia kiwango kisichozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa; Kusimamia deni la Taifa ili liendelee kuwa himilivu; kuhakikisha thamani ya shilingi ya Tanzania inatengamaa; Kuongeza thamani na mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi, kudhibiti matumizi ya fedha za kigeni na kuepuka kuagiza bidhaa zisizo za lazima kutoka nje ya nchi; na kuendelea kuwa na mikakati itakayowezesha kuwa na akiba ya fedha za kigeni zinazotosheleza kuagiza bidhaa na huduma nje bila ya matatizo.

19. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na mikakati nilioitaja hapo juu, majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango yatakayotekelawa ili kufikia azma ya kujenga msingi wa uchumi imara na Taifa linalojitegemea ni pamoja na:-
- i. Kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa;
 - ii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali;
 - iii. Kusimamia Deni la Taifa;
 - iv. Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kupunguza umaskini katika sekta mbalimbali;
 - v. Kusimamia mali ya Serikali;
 - vi. Kusimamia taasisi na mashirika ya umma;
 - vii. Kusimamia Sera ya Ubia kati ya Serikali na sekta binafsi;
 - viii. Kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu;
 - ix. Kudhibiti biashara ya fedha haramu pamoja na ufadhilli wa ugaidi;
 - x. Kuandaa, kusimamia na kutoa taarifa ya utekelezaji wa mipango ya kitaifa ya maendeleo; na
 - xi. Kusimamia sera, sheria, kanuni na taratibu za uhasibu, ukaguzi wa ndani na ununuzi wa umma.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2015/16

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, majukumu ya Wizara yaliendelea kutekelezwa kupitia mafungu tisa ya kibajeti na taasisi na mashirika 35 yaliyo chini yake (**Jedwali na.1**). Mafungu hayo ni Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango; Fungu 21 – Hazina; Fungu 22 - Deni la Taifa; Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 13 - Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu; Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina; Fungu 66 – Tume ya Mipango na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

21. ***Mheshimiwa Spika***, ili kufikia lengo kuu la kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla, Wizara katika mwaka 2015/16, pamoja na mambo mengine ilipanga kutekeleza yafuatayo:

- i. Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla;
- ii. Kuratibu Mipango ya Maendeleo ya Taifa;
- iii. Kuratibu Mikakati ya kupunguza Umaskini;
- iv. Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali;
- v. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
- vi. Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma;
- vii. Kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na uunganishaji wa mtandao wa malipo ya Serikali;
- viii. Kuendelea kulipa madeni ya ndani na nje kwa wakati;
- ix. Kusimamia Mali ya Serikali;
- x. Kusimamia Ununuzi wa Umma;
- xi. Kukagua hesabu za Serikali;
- xii. Kuimarisha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma;
- xiii. Kuendelea kuboresha huduma za pensheni kwa wastaa fu na malipo ya mirathi;
- xiv. Kudhibiti fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;
- xv. Kuishauri Serikali katika masuala ya fedha za Jamhuri ya Muungano yanayohusu matumizi ya kawaida katika Serikali zote mbili.

- xvi. Kupokea na kuchambua miradi ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi; na
- xvii. Kusimamia na kuratibu taasisi na mashirika ya umma chini ya Wizara;

3.1 Mapato kwa mwaka 2015/16

22. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya **shilingi bilioni 145.06** kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma. Hadi kufikia Machi, 2016 maduhuli yaliyokusanywa yalifikia **shilingi bilioni 129.92** sawa na asilimia 90 ya makadirio.

3.2 Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2015/16

23. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote Tisa iliidhinishiwa matumizi ya kawaida jumla ya **shilingi 7,317,624,478,770 (bilioni 7,317.62)**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 49,810,799,642 (bilioni 49.81)** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 7,267,813,679,128 (bilioni 7,267.81)** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ambapo kati ya hizo **shilingi 6,381,430,000,000 (bilioni 6,381.43)** ni Deni la Taifa. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya **shilingi 4,612,762,849,799 (bilioni 4,612.76)** zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kati ya hizo, mishahara ni **shilingi 29,675,454,380 (bilioni 29.67)**, sawa na asilimia 60 ya fedha zilizoidhinishwa; na matumizi mengineyo ni **shilingi 4,583,087,395,419 (bilioni 4,583.1)**, sawa na asilimia 63 ya fedha iliyoidhinishwa (**Jedwali Na.2**).

3.3 Matumizi kwa Miradi ya Maendeleo mwaka 2015/16

24. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi ya maendeleo, jumla ya **shilingi 1,031,758,764,000 (bilioni 1,031.76)** ziliidhinishwa kwa mafungu yote tisa ya

Wizara. Kati ya fedha hizo, **shilingi 658,637,200,000 (bilioni 658.64)** ni fedha za ndani na **shilingi 373,121,564,000 (bilioni 373.12)** ni fedha za nje. Hadi Machi, 2016, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya **shilingi 21,806,498,320 (bilioni 21.81)**. Kati ya hizo fedha za nje ni **shilingi 19,128,298,320 (bilioni 19.13)** na fedha za ndani ni **shilingi 2,678,200,000 (bilioni 2.68) (Jedwali Na.3)**.

3.4 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2015/16:

25. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kueleza mapato na matumizi ya Wizara napenda sasa kuchukua fursa hii kuelezea kwa kina utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2015/16.

3.4.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

26. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imesimamia utekelezaji wa Sera na Mikakati ya uchumi jumla zikiwemo Sera za Kibajeti na zile za Kifedha (Fiscal and Monetary policies) ili kuhakikisha kuwa uchumi wetu unaendelea kukua na hivyo kunufaisha wananchi walio wengi zaidi. Sera ya bajeti inalenga, pamoja na mambo mengine, kudhibiti na kupunguza mfumuko wa bei na hivyo kupunguza gharama za maisha ya wananchi.

3.4.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa

27. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu uandaaji na ufuatiliaji wa mipango ya maendeleo nchini sambamba na kusimamia uchumi. Ili kutekeleza majukumu hayo, Wizara imekamilisha uandaaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na tayari umeidhinishwa na Bunge lako tukufu. Aidha, Wizara imeandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Mpango huu ni wa kwanza katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17 – 2020/21.

28. **Mheshimiwa Spika**, mikakati maalum iliyozingatiwa katika Mpango wa Mwaka 2016/17 ni pamoja na:- Kuendelea kuandaa mazingira wezeshi kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, hususan miradi ya viwanda; kushawishi sekta binafsi za ndani na nje ya nchi kushiriki katika kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo; Kutoa mwongozo kwa sekta binafsi kushiriki katika miradi kwa njia ya ubia na sekta ya umma na; Kuweka mikakati ya kuvutia uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja.

29. **Mheshimiwa Spika**, katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16, Wizara imefanya uchambuzi wa maandiko ya miradi na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kila robo mwaka; na kufuatilia utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Kitaifa ya kimkakati. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *Overseas Development Institute* (ODI) iliendesha na kukamilisha tafiti kuhusu aina ya viwanda vitakavyopewa kipaumbele kwa kuzingatia fursa za Tanzania, kubaini malengo ya maendeleo ya viwanda kwa miaka 5 (2016/17 – 2020/21); maendeleo ya sayansi na teknolojia; na kubaini vyanzo vya mapato kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango. Tafiti hizo zimetumika kuboresha maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

3.4.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini

30. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa MKUKUTA-II ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mkakati huo ambao baada ya kuongezewa muda wa mwaka mmoja wa utekelezaji, unafikia ukomo wake mwezi Juni, 2016. Matokeo ya tathmini hiyo yameainishwa katika Taarifa ya Utekelezaji wa MKUKUTA-II kwa kipindi cha Miaka Mitano (2010-2015). Taarifa hii ilisambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge wakati nilipowasilisha mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili (2016/17 - 2020/21) kwenye semina ya

Waheshimiwa Wabunge mwezi Februari, 2016. Tathmini hiyo imetoa mchango mkubwa katika kubainisha vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo Awamu ya Pili ambao umejumuisha masuala ya kupambana na umaskini.

31. **Mheshimiwa Spika**, kwa ufupi, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa MKUKUTA-II ni pamoja na kukua kwa pato la wastani la Mtanzania kutoka shilingi 770,464.3 mwaka 2010 kufikia shilingi 1,918,928 mwaka 2015; kuongezeka kwa kasi ya kupungua kwa umaskini wa kipato ambapo kati ya mwaka 2007 na 2012 umasikini ulipungua kwa asilimia 6.2, kutoka asilimia 34.4 hadi asilimia 28.2, ikilinganishwa na kupungua kwa kiwango cha asilimia 4.6 katika kipindi cha miaka 15, yaani kutoka asilimia 39 mwaka 1992 hadi kufikia 34.4 mwaka 2007.

32. **Mheshimiwa Spika**, umri wa mtanzania wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 51 mwaka 2001 hadi miaka 61 mwaka 2012. Mafanikio hayo kwa pamoja yamechangia kupandisha Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu (Human Development Index - HDI) kutoka asilimia 48.8 mwaka 2014 hadi asilimia 52 mwaka 2015.

3.4.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

(a) Mapato ya Ndani

33. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Sera za Mapato zililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya **shilingi bilioni 13,999.52** (ikijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa). Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya makusanyo ya ndani (ikijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa) yalikuwa **shilingi bilioni 10,346.55** sawa na **asilimia 74** ya makadirio ya mwaka.

34. **Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha ukusanyaji wa mapato ya kodi, Wizara imeingia mikataba ya kiutendaji na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanzia ngazi ya juu mpaka wasimamizi wa chini; kupitia TRA, Wizara imeendelea kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD) ikiwa ni pamoja na kuanza kutoa mashine hizo bure kwa wafanyabiashara na kupiga marufuku Taasisi, Wakala wa Serikali, na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya biashara na wazabuni ambao hawatumii mashine hizo; kuboresha matumizi ya mfumo wa TANCIS pamoja na Mfumo Mmoja wa Ukadiriaji wa Thamani za Bidhaa; Kuwatambua walipa kodi kupitia tafiti mbalimbali na hatimaye kuwasajili; na Kutekeleza utaratibu wa ulipaji kodi kwa kutumia vitalu nya kodi.

35. **Mheshimiwa Spika**, hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na: kuwatambua na kuwasajili wajasiriamali walio kwenye sekta isiyo rasmi na kufuutilia mwenendo wa malipo yao; Kutekeleza mkakati wa ulipaji kodi kwa hiari; Kufanya utafiti kuhusu kodi za pango za majengo ambazo zinatoa mwelekeo wa kodi za mapato kutoka kwa wenye majengo ya biashara; Kutumia mifumo ya TEHAMA katika kusajili na malipo ya kodi; na uwasilishaji kwa njia ya kielektroniki wa Ritani za kodi ya ongezeko la thamani na miamala ya forodha. Aidha, Serikali ilikamilisha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015 yenyelengo la kuhakikisha kuwa matumizi ya mapato yatokanayo na mafuta na gesi yatasimamiwa ipasavyo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

36. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi Wizara imesimamia na kuhimiza utumiaji wa mfumo wa kielektroniki katika utoaji wa risiti kwa tozo, faini, ada na malipo mengine yote ya Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na mawakala wote wa Serikali. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza uongezaji wa kufanya uthamini wa majengo mijini ili kuhakikisha ulipaji wa viwango stahiki; na kusimamia kwa karibu zaidi mashirika ya umma na wakala wa serikali ili kuhakikisha Serikali inapata gawio stahiki, matumizi yasiyo na tija yanaondolewa na mapato ya ziada yanachangia mfuko mkuu wa Serikali.

(b) Misaada na Mikopo

37. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ililenga kuendeleza ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo Washirika wa Maendeleo katika kutekeleza mipango ya maendeleo. Katika mwaka 2015/16, Washirika wa Maendeleo waliahidi kuchangia bajeti ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi bilioni 2,322.5** ambapo misaada ya Kibajeti ni **shilingi bilioni 660**, Mifuko ya kisekta ni **shilingi bilioni 199** na miradi ya Maendeleo ni **shilingi bilioni 1,463**.
38. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2016 kiasi cha **shilingi bilioni 1,064.89** sawa na **asilimia 46** kimepokelewa. Kati ya kiasi hicho, Misaada ya kibajeti ni **shilingi bilioni 169.6** (sawa na asilimia 26 ya ahadi), Mifuko ya kisekta ni **shilingi bilioni 243.96** (sawa na asilimia 123 ya ahadi) na Miradi ya Maendeleo **shilingi bilioni 651.32** (sawa na asilimia 46 ya ahadi).
39. **Mheshimiwa Spika**, kupungua kwa misaada toka nje kunatokana na kujiondoa kwa baadhi ya Washirika wa Maendeleo wanaochangia kuititia Misaada na mikopo ya kibajeti na baadhi ya Washirika wa Maendeleo kupunguza ahadi zao. Wafadhili wanaochangia kuititia misaada ya kibajeti walipunguza michango yao kutoka **shilingi bilioni 660** mpaka **shilingi bilioni 399** katikati ya mwaka wa fedha 2015/16 na wengine kuhusisha utoaji wa fedha na masharti ambayo hayakuwemo katika makubaliano ya awali. Katika kushughulikia changamoto hizi, Serikali inaendelea na mazungumzo na Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha kwamba fedha zilizoahidiwa zinatolewa kwa wakati.

3.4.5. Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

40. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Wizara imeratibu uandaaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2016/17 pamoja na Kitabu cha Taarifa ya Hali ya uchumi kwa

mwaka 2015 na; kufanya marekebisho ya takwimu za Bajeti ya Mafungu mbalimbali kwenye mfumo wa IFMS na kuchapisha vitabu vya bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16 (Juzuu Na. II, III & IV). Aidha, Wizara iliandaa, kuchapisha na kusambaza kitabu cha tafsiri rahisi ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2015/16 yaani "Citizen's Budget"; na kuendesha mafunzo ya wakufunzi wa kitaifa wa Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali kwa Mikoa 26, Halmashauri 182, pamoja na Wizara zote nchini.

41. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha usimamizi wa bajeti hasa kwenye miradi ya maendeleo unazingatiwa, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa fedha za Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; mapato na matumizi ya VETA; fedha za 'Skills Development Levy' kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania. Aidha, Wizara ilihakiki madeni ya Shirika la Habari Tanzania (TBC), Kampuni ya magazeti Tanzania (TSN), Kampuni ya Simu (TTCL) yanayodaiwa katika Taasisi mbalimbali za Serikali na Shirika la kudhibiti nzige wa jangwani na nzige wekundu. Wizara pia ilifanya ufuatiliaji wa fedha za SDL zilizotolewa kwenye mradi wa "Support Skills Development Project" kwa Wizara ya Kazi.

3.4.6. Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma

42. **Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti matumizi ya fedha za umma, Wizara kuitia Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali imeendelea kufanya ukaguzi maalum katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Jukumu hilo limetekelizwa kwa kufanya uhakiki wa madai ya walimu na watumishi wasio walimu wa Serikali, watoa huduma ya chakula katika shule za msingi na sekondari za Serikali, madai ya Wakandarasi, Washauri, madai ya fidia, mirahaba na gharama za usimamizi wakati wa utekelezaji wa miradi ya barabara.

43. **Mheshimiwa Spika**, kaguzi nyingine zilizofanyika ni pamoja na ukaguzi maalum kuhusu matumizi ya fedha za umma katika kampuni ya Reli Tanzania (TRL), Ukaguzi maalum katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), ukaguzi wa ununuvi na ukaguzi

wa mikataba katika sekta ya umma, na Ukaguzi maalum wa kuthibitisha deni la ujenzi wa Jengo la Hospitali ya MOI (MOI Phase III). Matokeo ya kazi hizi yameiwezesha serikali kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 482.28 iwapo madeni hayo yangelipwa bila kuhakikiwa. Wizara imeendelea kutoa mapendekezo mbalimbali yanayotokana na matokeo ya kazi za ukaguzi maalum na kuwasilisha kwa Maafisa Masuuli kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki.

44. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia inaendelea kufanya ukaguzi wa mfumo wa malipo ya mishahara katika taasisi za Serikali; na ukaguzi wa kiufundi katika miradi kumi ya maendeleo katika mikoa ya Mbeya na Iringa. Miradi hii inahusisha majengo, barabara, maji na umwagiliaji. Miradi hiyo ni; nyumba 6,064 za watumishi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ujenzi wa hifadhi ya nyayo za kale huko Ngorongoro, mfumo wa maduhuli wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), na jengo la ofisi za kanda ya ziwa ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA). Wizara pia imefanya ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye taarifa za ukaguzi wa ndani pamoja na ufuatiliaji wa mapendekezo ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali.

45. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma imetua mafunzo ya muda mfupi juu ya usimamizi wa fedha za umma na maboresho kwa watumishi wa kada za uhasibu, ugavi, ukaguzi, na mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji; na imeratibu na kusimamia zoezi la Upimaji wa Mifumo ya Fedha (Public Expenditure and Financial Accountability - PEFA) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara imeratibu na kusimamia Mpango Maalum wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na; Kuratibu na Kusimamia Maboresho ya Usimamizi wa Fedha kwa Upande wa Zanzibar hasa Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mamlaka ya Mapato Zanzibar na Wizara ya Fedha ya Zanzibar.

3.4.7. Usimamizi wa Malipo

46. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kudhamini mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 238 wa kada ya uhasibu, ugavi, uchumi na kompyuta kutoka kwenye wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Manispaa, Halmashauri za miji; na Watumishi wapatao 650 wa kada ya uhasibu wamepatiwa mafunzo ya kutayarisha hesabu kwa kutumia viwango vya kimataifa vya Uhasibu (IPSAS Accrual). Aidha, Mfuko wa Bunge umeunganishwa kwenye Mtandao wa Malipo wa kieletroniki wa TISS pamoja na EFT; Malipo ya Mirathi (Death Gratuity) yameunganishwa kwenye mfumo wa "Electronic Fund Transfer". Mfumo huu umewezesha malipo kuingizwa kwenye akaunti za benki za warithi moja kwa moja na hivyo kuharakisha malipo. Wizara imeendelea kusimamia uendeshaji mtandao wa malipo wa Serikali (Integrated Financial Management System – IFMS) kwa kutoa ushauri wa kitaalamu na kuziwezesha Idara/Wizara za Serikali pamoja na Mikoa kutumia mtandao kwa ufanisi. Pia kutatua matatizo ya kiufundi pale yanapotokea.

3.4.8. Deni la Taifa

47. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia Deni la Taifa kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134. Aidha, msisitizo umewekwa kukopa mikopo yenye masharti nafuu ambayo inakopwa kwa uangalifu na kutumika kwenye miradi yenye vichocheo vya ukuaji wa uchumi, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, ujenzi wa mitambo ya kufua umeme na ujenzi wa viwanja vya ndege.

48. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2015/16, Serikali ilitenga shilingi bilioni 504.57 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la nje. Hadi Machi, 2016 shilingi bilioni 414.66 sawa na asilimia 82 zilitumika kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 899.89 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la ndani. Hadi Machi, 2016 shilingi bilioni 547.88 sawa na asilimia 61 zilitumika kwa ajili hiyo.

49. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2015/16 Serikali ilitenga pia shilingi bilioni 421.20 kwa ajili ya kulipa mtaji wa deni la nje. Hadi Machi, 2016 shilingi bilioni 395.90 sawa na asilimia 94 zilitumika kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali ilitenga shilingi trilioni 2.7 kwa ajili ya kulipa mtaji wa deni la ndani. Hadi Machi, 2016 shilingi trilioni 1.86 sawa na asilimia 69 zilitumika kwa ajili hiyo.

3.4.9. Usimamizi wa Mali ya Serikali

50. **Mheshimiwa Spika**, katika jukumu la usimamizi wa mali ya Serikali, Wizara imefanya uthamini wa ardhi, majengo na mali nyingine za Serikali ambapo taasisi kumi zinaendelea kufanyiwa uthamini; Kuondosha mali chakavu katika Wizara na Idara za Serikali ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.06 zilikusanywa kutokana na mauzo ya magari na vifaa chakavu; na vibali vyta uondoshaji wa mali chakavu vilivyokuwa na thamani ya shilingi bilioni 1.68 vilitolewa kwa mamlaka na taasisi mbalimbali za Serikali.

3.4.10. Ununuzi wa Umma

51. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16 Wizara imepitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.7 ya Mwaka 2011 na kupendekeza marekebisho ya sheria hiyo; Kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma na mkakati wa utekelezaji wake; Kuanza kutekeleza mpango wa mahitaji ya mafunzo wa maafisa ununuzi na ugavi kwa kuwajengea uwezo wa namna ya kupunguza vihatarishi katika ununuzi wa umma; Kuhakiki taarifa za maafisa ununuzi na ugavi na kuziweka katika daftari la maafisa ununuzi na ugavi Serikalini pamoja na kukamilisha maandalizi ya kufanya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa umma nchini.

52. **Mheshimiwa Spika**, katika usimamizi wa ununuzi wa umma, Wizara kuitia Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma imefanya uchunguzi katika zabuni 26 zinazohusu manunuzi yaliyofanywa na taasisi mbalimbali za umma. Kati ya hizo, taarifa za

uchunguzi wa zabuni 18 zimekamilika na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika, na zabuni 8 zilizobaki bado zinaendelea kufanyiwa uchunguzi. Aidha, Wizara imefanya ukaguzi wa taratibu za utoaji wa zabuni na utekelezaji wa miradi na mikataba itokanayo na ununuzi wa umma kwa taasisi 126, zikiwemo Wizara na Idara zinazojitegemea 23, mashirika ya umma 36 na Serikali za Mitaa 67. Ukaguzi huu umehusisha jumla ya mikataba 5,206 yenye thamani ya shilingi bilioni 420.01. Maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu kwa ukaguzi uliofanyika ni katika usimamizi wa mikataba, utunzaji wa nyaraka, utumiaji wa mfumo wa uwasilishaji wa taarifa za ununuzi kwa njia ya kieletroniki pamoja na kushughulikia malalamiko ya wazabuni.

53. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanya kaguzi katika miradi ya ujenzi 385 inayotekelawa na taasisi 126. Miradi hiyo imejumuisha barabara, madaraja, majengo, ukarabati wa reli, ununuzi wa vifaa pamoja na huduma za Washauri Waelekezi. Maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu ni pamoja na ukosefu wa michoro na usanifu (design and drawings), malipo ya ziada kwa kazi ambazo hazikufanyika, kuzidisha vipimo vya kazi husika, kutoteua wasimamizi wa miradi, kutoandaa taarifa za utekelezaji wa miradi na kutoambatanisha hati za malipo na vipimo halisi (payment certificates and measurement sheets) ili kuthibitisha uhalali wa malipo husika.

54. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imezifungia jumla ya kampuni 21 (pamoja na wakurugenzi wake), kushiriki katika zabuni zinazohusu manunuzi ya umma kwa kipindi cha mwaka mmoja. Asilimia 90 ya kampuni zilizofungiwa (kampuni 19) ilisababishwa na kutotimiza masharti ya mkataba katika utekelezaji wa miradi husika na asilimia 10 iliyobaki (kampuni 2) zilifungiwa kutokana na kuwasilisha nyaraka zisizo halali wakati wa mchakato wa zabuni.

55. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa ununuzi nchini, Wizara imeendelea kupokea taarifa za manunuzi kutoka kwa taasisi nunuzi 388, kati ya 475 zilizounganishwa kwenye mfumo wa utunzaji wa taarifa za manunuzi, yaani 'Procurement Management Information System'. Aidha Wizara

imeufanyia maboresho mfumo huu ili kurahisisha zaidi shughuli za ununuzi nchini, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wakaguzi wa ndani wa taasisi zote za umma kuutumia mfumo katika kutoa taarifa za utekelezaji wa sheria ya manunuzi kwenye taasisi zao.

56. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma iliendelea kusikiliza na kutatua mashauri yanayotokana na ununuzi wa umma. Hadi Machi, 2016 jumla ya mashauri 30 yalipokelewa. Kati ya hayo, mashauri 18 walalamikaji walishinda, mashauri 11 Serikali ilishinda na lalamiko moja lilifutwa na mlalamikaji.

57. **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha huduma ya ununuzi Serikalini, Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini iliendelea na utaratibu wa kununua magari kwa pamoja kwa lengo la kupunguza ghamama. Hadi Machi, 2016 Serikali imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 16.61 kwa kununua magari 551 kwa kutumia utaratibu huu. Aidha, Wizara imeongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi mafuta kwa kujenga kituo kipyta katika Wilaya ya Ileje mkoani Mbeya chenye ujazo wa lita 50,000. Wizara imetoe mafunzo kwa taasisi 11 katika mkoa wa Dar Es Salaam kuhusu namna ya kutumia mfumo wa udhibiti wa usimamizi wa mafuta ya magari na mpaka sasa taasisi tatu ambazo ni PPRA, PSPTB na GPSA zimeanza kutumia mfumo huu.

58. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi imesajili jumla ya Wataalamu 1,735 wa fani ya ununuzi na ugavi kati ya wataalam 1,250 iliyokusudia kusajili kwa mwaka 2015/16. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya wataalam waliosajiliwa na Bodi katika ngazi mbalimbali imefikia 5,187. Aidha, Bodi iliendesha mitihani ya taaluma ya ununuzi na ugavi katika ngazi mbalimbali ambapo kwa mwaka 2015/16, jumla ya watahiniwa 1,651 walifanya mitihani na watahiniwa 707 sawa na asilimia 42.8 walifaulu. Vilevile, Bodi ilizindua mitaala mipya ya mafunzo ya taaluma ya ununuzi na ugavi ambapo itaanza kufundishwa mwaka 2016/17.

59. **Mheshimiwa Spika**, majukumu mengine yaliyotekelawa na Bodi ni pamoja na:- Kufanya ukaguzi wa wanataaluma wenyе sifa za kufanya kazi za ununuzi na ugavi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria kwenye taasisi 50 katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Lindi; na kukamilisha marekebisho ya Kanuni Na.GN.364 na GN.365 za mwaka 2009 ili ziendane na marekebisho ya sheria Na. 23 ya mwaka 2007 ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi wa Bodi.

60. **Mheshimiwa Spika**, Bodi imefanikiwa kusajiliwa na taasisi ya kimataifa ya "International Federation of Purchasing and Supply Management" na kupata – "Global Standards Certification". Hili limefanikiwa baada ya uchambuzi uliofanywa wa mitaala ya Bodi kuonekana imekidhi vigezo vya usajili huo wa kimataifa. Hii inafanya wataalamu wanaofanya mitihani ya Bodi na kufaulu kupata sifa ya kukubalika kimataifa, hivyo kuwa na nafasi kubwa ya ushindani katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

3.4.11. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

61. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ilifanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2014/15 kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi wa hesabu za Wizara na Idara za Serikali zinazojitegemea 63, mikoa 25 ya Tanzania Bara; Wakala za Serikali 32, Mifuko maalum na Taasisi nyingine za Serikali 45, Balozi 34 za Tanzania nje ya nchi, na hivyo kufanya jumla ya Taasisi zote zilizokaguliwa chini ya Serikali Kuu kufikia 199. Ukaguzi mwingine ulifanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 164 na Mashirika ya Umma 102 kati ya Mashirika 186.

62. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa miradi ya maendeleo, jumla ya ripoti 799 za ukaguzi zimetolewa. Miradi hii ni ile inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, na ile inayogharamiwa kwa fedha za maendeleo za ndani. Aidha, katika ukaguzi wa ufanisi,

jumla ya ripoti 11 zimetolewa katika kipindi kilichoishia Machi, 2016. Kwa ujumla, ukaguzi uliofanyika katika mwaka wa fedha 2014/15 umewezesha kutolewa Ripoti kuu 5 ambazo zimewasilishwa kwenye Bunge lako hili tukufu, tarehe 25 Aprili, 2016. Ripoti hizo ni muhtasari wa jumla ya ripoti 1,275 zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka 2014/15.

63. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti za ukaguzi wa fedha zilizotolewa miaka iliyopita. Katika kipindi hicho kulikuwa na mapendekezo 99 yaliyotolewa kwa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma. Kati ya hayo, yaliyotekelawa ni 35 sawa na asilimia 35. Aidha, utekelezaji wa mapendekezo 11 bado haujaanza na wa mapendekezo 53 unaendelea. Kwa ujumla, Mashirika ya Umma yametekeliza mapendekezo yote yaliyotolewa. Aidha, Serikali Kuu imeonesha juhudini nzuri katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa kuwa ni asilimia mbili tu ya mapendekezo ndiyo yaliyokuwa hayajatekelezwa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeonekana kutotekeliza mapendekezo hayo kwa kiwango cha asilimia 63. Kwa upande wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti za ukaguzi wa ufanisi, kati ya mapendekezo 113 yaliyotolewa mapendekezo 29 yalitekelezwa, 68 yapo kwenye hatua za utekelezaji; na 16 hayajatekelezwa.

64. **Mheshimiwa Spika**, matokeo ya ukaguzi uliofanyika katika mwaka 2014/15 umeonesha kuwa, kati ya taasisi 1,264 zilizokaguliwa, hati safi zilizotolewa ni 1,065; hati zenye shaka 194; hati zisizoridhisha 4; na hati mbaya 2. Aidha, kati ya hati safi 1065 zilizotolewa, hati 739 zilihusu miradi ya maendeleo. Vilevile, hati zenye shaka 60 zilitolewa kwenye miradi ya maendeleo. Hakuna miradi iliyopata hati zisizoridhisha au hati mbaya. Serikali Kuu ilipata jumla ya hati safi 180, hati zenye shaka 18, hati isiyoridhisha moja, na haikupata hati mbaya. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipata hati safi 47, hati zenye shaka 113, hati zisizoridhisha 3 na hati mbaya moja. Aidha, Mashirika ya Umma yalipata hati safi 99, hati zenye shaka 3, na hakuna hati isiyoridhisha wala hati mbaya.

3.4.12. Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma

65. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kusimamia rasilimali za Serikali kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali kwa ujumla. Rasilimali hizi ni pamoja na uwekezaji wa Serikali katika hisa za Mashirika ya Umma na ya Binafsi. Aidha, katika kutekeleza jukumu hili, Wizara husimamia utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma na kutoa ushauri kwa Serikali juu ya uwekezaji wake na nini kifanyike ili kuimarisha uendeshaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma yanayosimamiwa na Wizara yapatayo 216.
66. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hili, Wizara kwa mwaka 2015/16 imekamilisha Taarifa ya uwekezaji wa Serikali kwenye Mashirika na Taasisi za Umma na kuiwasilisha kwa Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - CAG; Kukirejesha kwenye umiliki wa Serikali Kiwanda cha *General Tyre* kwa kununua hisa za mbia; Kukamilisha uhakiki wa madai wa waliokuwa watumishi kwenye mashirika yaliyobinafsishwa; Kufanya Ukaguzi wa Kimenejimenti kwenye Taasisi nne ambazo ni Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Kivukoni, Shirika la Elimu - Kibaha, Bodii ya Kahawa Tanzania na Chuo cha Ubaharia – Dar Es Salaam ambapo taarifa ya kaguzi hizo zimeandaliwa.
67. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia ilifanya uperembaji (Monitoring and Evaluation) kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma 55 yaliyobinafsishwa kwa lengo la kukagua ufanisi na kuhakiki utekelezaji wa masharti kulingana na mikataba ya ununuzi kwa mujibu wa agizo la Mheshimiwa Rais wakati wa ufunguzi wa Bunge la 11. Baadhi ya mashirika hayo ni Mwanza Textile, Shinyanga Meat, Ilemela Fisheries, Manawa Ginneries, Blanket Manufacturing, Mtwara Cashewnut Factory, Likombe Cashewnut, Newala I Cashewnut Factory, Newala II Cashewnut Factory, Mtama Cashewnut Factory, Mufindi Pyrethrum Factory, TTA Dabaga, Mufindi Tea Company, Ludodolelo Pyrethrum Factory na Mahenye Farm.

3.4.13. Mafao ya Wastaifu na Mirathi

68. **Mheshimiwa Spika**, Dhana ya msingi ya sekta ya hifadhi ya jamii imejikita katika kuhakikisha kuwa wananchi wanawezeshwa kuishi maisha yenyestaha kwa kupata huduma za msingi katika vipindi vya uzee, kifo, maradhi, ukosefu wa kazi, uzazi na hali nyingine itakayosababisha mtu asiweze kufanya shughuli za kujiongezea kipato. Serikali kwa kutambua mchango mkubwa uliotolewa na wastaifu katika ujenzi wa Taifa imeendelea kuboresha huduma ya malipo kwa wastaifu, kwa kulipa pensheni moja kwa moja kwenye akaunti zao kwa kutumia mfumo wa TEHAMA wa Benki Kuu ya Tanzania uitwao TACH kuanzia mwezi Mei, 2015. Aidha kumbukumbu za wastaifu zimeendelea kuhifadhiwa kwenye mfumo wa TEHAMA unaoitwa SAPERION ambapo hadi Machi, 2016 kumbukumbu za wastaifu 66,666 zilikuwa zimewekwa kwenye mfumo huo.

69. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kutambua umuhimu huo wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa Umma na kwa kuzingatia sheria na kanuni za mifuko ya hifadhi ya jamii, Wizara hadi Machi, 2016 iliwasilisha mchango wa mwajiri kiasi cha shilingi bilioni 274.0.

3.4.14. Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi

70. **Mheshimiwa Spika**; katika mwaka 2015/16 Wizara kuitengi Kitengo cha Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu. Hadi kufikia Machi, 2016 Wizara imepokea na kuchambua taarifa 164 za miamala shuku inayohusu fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi. Kati ya hizo, taarifa 52 za kiintelijensia ziliwasilishwa kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa uchunguzi. Aidha, Wizara ilikagua watoa taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na benki 17 na kampuni ya masoko ya hisa moja.

71. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia ilisaini hati za makubaliano (Memorandum of Understanding) na wadau wa ndani na nje ya nchi ikiwemo Taasisi ya Kuzuia na

Kupambana na Rushwa na Kitengo cha Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu cha Zimbabwe na hivyo kufanya idadi ya hati za makubaliano na vitengo mbalimbali kuwa kumi; Kutoa elimu na mafunzo kwa wadau mbalimbali wakiwemo watoa taarifa za jinsi ya kutumia mfumo maalum wa uchambuzi wa taarifa wa kompyuta kwa ajili ya kurahisisha uwasilishaji wa taarifa za miamala shuku na uchambuzi; na Kuratibu na kusimamia zoezi la Kitaifa la kutathmini viashiria hatarishi vyta fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

3.4.15. Tume ya Pamoja ya Fedha

72. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16 Wizara kuititia Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha Ripoti ya Stadi kuhusu Mwenendo wa Uchumi na Mapato ya Muungano ambayo lengo lake ni kuiwezesha Tume kushauri na kupendekeza namna bora ya kuboresha vyanzo vyta mapato ya muungano kwa kuzingatia mwenendo wa uchumi. Ripoti ya stadi hiyo imewasilishwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

3.4.16. Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi

73. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kupokea na kuchambua miradi ya ubia kwa lengo la kuiidhinisha kwa mujibu wa Sheria. Wizara kuititia kitengo chake cha ubia kati ya sekta ya umma na sekta Binafsi imechambua na kuidhinisha mradi wa kufua umeme wa Kinyerezi III. Aidha, upembuzi yakinifu wa mradi wa barabara ya tozo kati ya Dar es Salaam na Chalinze unaendelea kufanyika. Kadhalika, Serikali ipo katika hatua ya mwisho kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya mradi wa kuzalisha madawa muhimu na utengenezaji wa vifaa tiba chini ya Bohari Kuu ya Madawa (MSD). Vilevile, Wizara kuititia kitengo chake cha ubia inafanya uchambuzi wa maandiko ya mradi wa daraja la Kigamboni kwa lengo la kuidhinisha Mradi huo tayari kwa kuandaliwa mkataba wa uendeshaji.

74. **Mheshimiwa Spika**, Sambamba na uchambuzi wa miradi, katika mwaka 2015/16 mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa makundi sita yakiwemo watunga sera; Maofisa waandamizi Serikali Kuu na Serikali za Mitaa; Taasisi Binafsi; Mashirika ya Umma; Taasisi za Serikali; na taasisi za fedha kutegemea na mahitaji na majukumu ya kila kundi. Jumla ya wadau 217 walipatiwa mafunzo kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Miradi ya Ubia.

3.5. USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA

75. **Mheshimiwa Spika**, Naomba sasa uniruhusu kueleza utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2015/16 kama ifuatavyo:-

3.5.1. Huduma za Kibenki

(i) Benki Kuu ya Tanzania – BoT

76. **Mheshimiwa Spika**, Jukumu la msingi la Benki Kuu ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuwa na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei kwa ajili ya ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa. Ili kufanikisha azma hii, Benki Kuu inadhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa kutumia nyenzo mbalimbali ambazo ni: Kuza dhamana na hati fungani za Serikali; Kukopa au kukopesha mabenki kwa muda mfupi; Kuza fedha za kigeni katika soko la jumla la mabenki; Kurekebisha riba inayotozwa kwa mabenki na Serikali yanapokopa toka Benki Kuu; na Kuagiza mabenki kisheria yaweke sehemu ya amana za wateja wake Benki Kuu. Lengo ni kudumisha utulivu wa uchumi mpana na kuongeza ufanisi katika shughuli za uzalishaji kwa ajili ya ukuaji mzuri na endelevu wa uchumi.

77. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kilichoishia Machi, 2016 mfumuko wa bei umeshuka hadi kufikia asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwezi Disemba, 2015. Aidha, wastani wa mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula na nishati, ambao hupima

kwa usahihi zaidi utekelezaji wa sera ya fedha, umeendelea kubaki katika kiwango cha chini cha asilimia 2.8 mwezi Machi, 2016. Hii inatokana na hatua mbalimbali thabiti za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania katika kudhibiti ujazi wa fedha na ukwasi katika uchumi.

78. **Mheshimiwa Spika**, Ongezeko la fedha taslimu ambacho ni kipimo bora cha ukwasi kwenye uchumi katika kipindi kilichoishia Machi, 2016 ulikua kwa wastani wa asilimia 12.1 uliokuwa ndani ya lengo la asilimia 17.1. Sekta ya fedha imeendelea kuchangia ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa kasi nzuri ya kutoa mikopo kwa wakati na kwa kiwango cha kutosha. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 24.0 katika mwaka ulioishia mwezi Februari, 2016, ikilinganishwa na makadirio ya asilimia 19.3 kwa mwaka 2015/16. Mikopo mingi kwa sekta binafsi ilielekezwa kwenye shughuli za biashara iliyokuwa na asilimia 19.4 ya jumla ya mikopo yote, shughuli binafsi asilimia 17.6, uzalishaji viwandani asilimia 11.1, shughuli za kilimo asilimia 7.8 na uchukuzi na mawasiliano asilimia 7.8.

79. **Mheshimiwa Spika**, Benki Kuu ina jukumu pia la kusimamia huduma za kibenki ambapo sekta hii imeendelea kukua ikichangiwa na uanzishwaji wa taasisi mpya za kifedha ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Hadi kufikia Machi, 2016, kulikuwa na jumla ya benki na taasisi za fedha zinazosimamiwa na Benki Kuu zipatazo 63 zenye matawi 725 nchini kote. Kiwango cha mitaji ikilinganishwa na mali iliyowekezwa kilikuwa asilimia 18.11 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachotakiwa kisheria cha asilimia 12.0. Kiwango cha mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu ikilinganishwa na kiwango cha amana zinazoweza kuhitajika katika muda mfupi kilifikia asilimia 36.84 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachohitajika kisheria cha asilimia 20.

80. **Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wasiofikiwa na mabenki umeendelea kuongezeka kutokana na ubunifu wa mipango ya utoaji wa huduma za malipo ya rejareja kuitia simu za mikononi, pamoja na huduma za

uwakala wa mabenki. Ubunifu huu umechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la amana za watu binafsi ambazo zimefikia shilingi trilioni 18.2 mwezi Machi, 2016 kutoka shilingi trilioni 15.6 mwezi Machi, 2015.

81. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Mifumo ya Malipo Nchini (National Payment Systems Act, 2015) imekamilika na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali sheria na kanuni zinazohusu utoaji wa leseni na kuridhia uanzishwaji wa mifumo ya malipo nchini, pamoja na kanuni zake. Pia maboresho katika mfumo mpya wa malipo kwa kutumia hundi (Tanzania Automated Clearing System) ulioanza kutumika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2015, umeongeza ufanisi mkubwa na kupunguza muda wa kusubiria malipo ya hundi kutoka siku tatu mpaka saba hadi kufikia siku moja.

(ii) **Benki ya Maendeleo ya Kilimo -TADB**

82. **Mheshimiwa Spika**, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilipata leseni ya kujiendesha kama taasisi ya fedha ya kimaendeleo kutoka Benki Kuu ya Tanzania tarehe 4 Agosti 2015 na kuzinduliwa Rasmi na Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 8 Agosti, 2015. Madhumuni makuu ya kuanzishwa benki hii ni kusaidia upatikanaji, utoshelezi na usalama wa chakula endelevu nchini na kusaidia katika kuleta mapinduzi ya kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kilimo cha biashara ili kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

83. **Mheshimiwa Spika**, Serikali hadi sasa imeipatia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania mtaji wa shilingi bilioni 60. Aidha, katika hatua za awali, benki imeainisha minyororo 14 ya thamani ya mazao ya kilimo katika sekta ndogo ndogo nane itakayopewa kipaumbele katika kutoa mikopo kwa kuanzia. Sekta hizo ni za uzalishaji wa nafaka; mifugo; ufugaji wa samaki, kilimo cha matunda, maua, mbogamboga, na viungo; mazao ya viwanda hasa miwa na korosho; mbegu za uzalishaji mafuta ya kula; na mazao ya misitu hasa ufugaji wa nyuki na mazao yake.

84. ***Mheshimiwa Spika***, Benki imevijengea uwezo vikundi vipatavyo 89 vyenye jumla ya Wakulima 21,526 kwa ajili ya kuviardaa kuweza kuandika andiko la mkopo na kuweza kukopa. Hadi kufikia Machi, 2016, jumla ya vikundi nane mkoani Iringa vyenye wakulima 857 ndivyo vilivyoweza kukamilisha taratibu za ukopaji ambapo viliweza kupatiwa mkopo wa zaidi ya shilingi bilioni moja. Aidha, kwa sasa benki inaendelea na uchambuzi wa maombi mapya ya mikopo ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2016 benki imechambua maombi kutoka vikundi 51 vya wakulima yenyе jumla ya shilingi bilioni 39.

(iii) Benki ya Maendeleo TIB – TIB DFI

85. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi, 2016 Benki ya Maendeleo TIB imefadhili miradi mikubwa ya maendeleo hasa katika sekta ya miundombinu na viwanda. Miradi hii ni pamoja na mradi wa TPDC wa kuchakata na usafirishaji gesi asilia hadi kwenye mitambo ya TANESCO ya kufua umeme ya Kinyerezi/Dar es Salaam; Ujenzi wa njia ya umeme kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi; Mradi wa kuchakata gesi asilia wa kampuni ya Wentworth; Mradi wa maboti katika kuimarisha usimamizi wa uchimbaji gesi katika bahari ya Hindi; na Kiwanda cha kusindika kahawa laini (instant coffee) mjini Bukoba na Shirika la Reli Tanzania.

86. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka ulioishia Disemba, 2015 Benki ilipata faida ya shilingi bilioni 9.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 10.4 zilizopatikana mwaka 2014. Kupungua kwa faida kumetokana na mgawanyo wa rasilimali (assets) za kibiashara katika TIB Development Bank na kampuni yake tanzu ya TIB Corporate Bank. Waraka mizania uliongezeka kwa asilimia 32 hadi kufikia shilingi bilioni 689.0 Disemba, 2015, ikilinganishwa na shilingi bilioni 413.0 Disemba, 2014.

(iv) Benki ya Biashara TIB – TIB CBL

87. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wake wa kwanza wa kiutendaji, Benki ya Biashara TIB imepata faida ghafi (iliyokaguliwa) ya shilingi bilioni 5.3. Faida hii imetokana na mfumo imara na uadilifu wa udhibiti wa gharama za uendeshaji ambao kwa mjumuisho umeleta ufanisi mkubwa na kufanya matumizi ya benki kuwa madogo. Benki pia imeweza kupata mapato katika ubadilishaji fedha za kigeni kiasi cha shilingi bilioni 1.9. Mafanikio mengine yaliyopatikana katika mwaka 2015 ni pamoja na: kupatikana kwa leseni ya uendeshaji biashara ambayo imetolewa na Benki Kuu Julai, 2015; kuanzisha mfumo wa ulipaji kwa kutumia hundi na kuingia katika mfumo wa kitaifa wa kibenki wa kupitisha hundi kwa haraka (Cheque Truncation) ikiwa ni pamoja na mfumo wa kisasa wa kuweka na kutoa pesa kupitia simu za mkononi (mobile banking) ambavyo vitaifanya benki kuwa ya ushindani na ufanisi kibiashara; na uanzishwaji wa kitengo cha wateja wa hadhi (Premier Customers) katika matawi ya benki na kuhamisha matawi mengine ili kuweza kuwafikia wateja kwa njia bora zaidi.

(v) Benki ya Posta Tanzania - TPB

88. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, Benki ya Posta iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kibiashara kwa kusambaza huduma zake kwa wananchi. Hadi kufikia Machi, 2016 amana za wateja Benki ya Posta ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 312.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 240 Disemba, 2014. Thamani ya mikopo inayotolewa kwa wateja iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 254.36 ikilinganishwa na shilingi bilioni 196 Disemba, 2014. Pato ghafi lililozalishwa na benki liliongezeka na kufikia shilingi bilioni 73.95 Disemba, 2015 ikilinganishwa na shilingi bilioni 52.77 Disemba, 2014.

89. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2015 benki ilianza kutoa huduma kwa vikundi, hii ikiwa ni huduma mpya sokoni. Vikundi hivi ni pamoja na vikundi vya kuweka na kukopa vijijini. Hadi Machi, 2016 benki ilikuwa na wateja 2,617 na amana za thamani ya shilingi milioni 373. Aidha, benki ilianzisha utoaji huduma kwa VICOBA ambapo hadi

Machi, 2016 benki ilikuwa na wateja 26,276 na amana zenye thamani ya shilingi bilioni tatu. Benki ilitoa huduma kwa vikundi visivyo rasmi na kufikisha wateja 1,000 sambamba na amana za thamani ya shilingi milioni 880. Akaunti maalum kwa mashabiki wa timu za Simba, Yanga na Mbeya City zilikuwa na wateja 16,000 na amana zenye thamani ya shilingi bilioni moja.

(vi) Benki ya Twiga - Twiga Bancorp

90. ***Mheshimiwa Spika***, Benki ya Twiga imeendelea kutoa huduma mbalimbali za kibenki kupitia matawi yake matano na matawi madogo manne ambapo hadi Machi, 2016 amana za wateja ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 94.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 63.5 Juni, 2015 ikiwa ni ongezeko la asilimia 30. Aidha, mikopo iliyotolewa kwa wateja ilifikia shilingi bilioni 42.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 36.3 Juni, 2015 ikiwa ni ongezeko la asilimia 17. Vile vile, benki imewekeza kiasi cha shilingi bilioni 36.4 kwenye Dhamana za Serikali na Amana katika benki nyingine ikilinganishwa na shilingi bilioni 14.6 kama ilivyokuwa Juni, 2015 sawa na ongezeko la asilimia 149.

91. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016 Benki imepanga kuongeza amana za wateja kutoka shilingi bilioni 94.2 hadi kufikia shilingi bilioni 146.9; Kuwekeza kiasi cha shilingi bilioni 61.6 katika Dhamana za Serikali na Amana za muda maalumu kwenye mabenki ifikapo tarehe 31 Disemba, 2016 ikilinganishwa na Dhamana pamoja na Amana zenye thamani ya shilingi bilioni 39 kama ilivyokuwa kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Disemba, 2015 ambalo ni ongezeko la shilingi bilioni 22.6 au asilimia 58.

3.5.2. Mifuko ya Hifadhi za Jamii

(i) Mifuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma – PSPF

92. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Mifuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma umesajili jumla ya wanachama 465,198

ikilinganishwa na wanachama 429,759 waliokuwa wamesajiliwa hadi mwezi Juni, 2015. Aidha, katika kipindi hicho, kiasi cha shilingi bilioni 677.18 kilikusanywa kutoka kwenye vyanzo vyake ikiwemo shilingi bilioni 458.57 kutokana na michango ya wanachama, shilingi bilioni 83.25 kutoka Serikalini kwa ajili ya kulipia "Pre July, 1999", shilingi bilioni 21.3 mapato kutokana na uwekezaji katika vitega uchumi mbalimbali, shilingi bilioni 80.31 kutokana na vitega uchumi vilivyo komaa, shilingi bilioni 32.26 kutokana na marudisho ya mikopo kutoka kwa wanachama na shilingi bilioni 1.49 ni mapato kutokana na vyanzo vingine mbalimbali.

(ii) Mfuko wa Mafao ya Kustaaifu – GEPF

93. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Mfuko wa GEPF umesajili jumla ya wanachama 15,643. Katika kipindi hicho Makusanyo ya michango kutoka kwa wanachama yalifikia shilingi bilioni 44.48 sawa na asilimia 67 ya malengo ya mwaka mzima. Aidha, mapato ya vitega uchumi yameongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 21.41 sawa na asilimia 61 ya lengo. Vile vile, Thamani ya Mfuko ilifikia shilingi bilioni 384.5.

(iii) Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma – PPF

94. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma umesajili wanachama 49,828 na kufanya idadi ya wanachama kuongezeka na kufikia wanachama 242,530. Aidha, katika kipindi hicho kiasi cha shilingi bilioni 395.7 zilikusanywa ikiwa ni michango ya wanachama na mapato yatokanayo na uwekezaji. Thamani ya Mfuko imeongezeka kufikia shilingi trilioni 2.27 ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.9 ikilinganishwa na thamani ya Mfuko ya shilingi trilioni 2.08 iliyokuwa Juni, 2015. Ongezeko hilo lilitokana na kiasi cha uwekezaji katika makundi ya uwekezaji, kuongezeka kwa thamani ya hisa za kampuni

ambazo Mfuko umewekeza, ukusanyaji wa michango na mapato yatokanayo na uwekezaji.

3.5.3. Rufani za Kodi

95. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB) imesajili jumla ya kesi 167 ambapo kiasi cha kodi kinachobishaniwa ilikuwa shilingi bilioni 379.84 na Dola za Kimarekani milioni 26.72. Jumla ya rufaa 141 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi. Aidha, katika kipindi hicho Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) limesajili kesi 46. Kati ya hizo kesi 31 zenye kiasi cha fedha shilingi 7,878,419,937 na Dola za Kimarekani 43,503,018 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi.

3.5.4. Huduma za Bima

(i) Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima – TIRA

96. ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imeandaa Sera ya Bima ya Taifa ambayo iko katika hatua za mwisho kukamilishwa. Lengo kuu la sera hii ni kupanua wigo wa shughuli za bima nchini ili wananchi walio wengi waweze kunufaika na huduma za bima. Aidha, Mamlaka imefungua ofisi yake ya kanda mkoani Dodoma inayohudumia mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida na Tabora hivyo kufanya Mamlaka kufikisha ofisi za kanda tano ikiwa ni pamoja na Zanzibar, Arusha, Mwanza na Mbeya. Mamlaka pia imeendelea kupokea na kuyatolea ufumbuzi malalamiko ya wateja wa Bima ili kukuza imani kwa Wananchi kuhusu huduma za Bima kuitia Baraza la usuluhishi la Bima.

(ii) Shirika la Bima la Taifa – NIC

97. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi Machi, 2016 utendaji wa Shirika la Bima la Taifa kibiashara uliendelea kuimarika ambapo Shirika limekusanya

mapato ya shilingi bilioni 34.17. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 28.32 ni mapato yaliyotokana na ada za bima, shilingi bilioni 4.68 ni mapato yatokanayo na vitega uchumi, na shilingi bilioni 1.17 ni mapato yanayotokana na deni la mauzo ya nyumba. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya taasisi 15 za Serikali zilijiwekea bima kuitia Shirika la Bima la Taifa. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Bandari Tanzania; Benki Kuu ya Tanzania; Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam; Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania; Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro; Shirika la Bima la Zanzibar; Mamlaka ya Kudhibiti Chakula na Dawa; Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania; Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali; Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii; Mfuko wa Pensheni wa PSPF; Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar Es Salaam; Chuo cha Taifa Cha Usafirishaji; Taasisi ya Saratani Ocean Road; na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima.

98. **Mheshimiwa Spika**, Shirika lilisaini mkataba wa kujiunga katika mfumo wa Bima unaoziunganisha kampuni za Bima za nchi wanachama wa jumuiya ya COMESA unaojulikana kama “Intersurity Agreement” mwezi Machi, 2015. Makubaliano hayo yanaziwezesha nchi kuwa washiriki rasmi katika mpango wa himaya moja ya forodha kwa ukanda huu wa Afrika. Kwa kujiunga na mfumo huu, NIC itakuwa kampuni pekee yenye kubeba dhamana ya utoaji wa bima kwa mizigo yote itakayopita Tanzania kwa kuitia mpango wa “Regional Customs Transit Guarantee Scheme – RCTG”. Mpango huu umeliwezesha shirika kujiongezea mapato na kufaidika kuitia mfumo wa usafirishaji wa njia ya kati ujulikanao kama “Central Corridor” ambapo katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi, 2016 Shirika lilikusanya shilingi bilioni 1.52.

3.5.5. Mitaji na Dhamana

(i) Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana – CMSA

99. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kilichoishia Machi, 2016 kumekuwa na maendeleo ya kuridhisha katika masoko ya mitaji na uanzishwaji wa soko la bidhaa nchini. Idadi

ya makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Mitaji la Dar es Salaam iliongezeka kutoka 21 hadi 23 kufuatia kuorodheshwa kwa Benki ya Walimu ambayo iliongeza idadi ya wawekezaji katika soko hilo kutoka 200,000 hadi 435,000.

100. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ilitoa idhini ya kuuzwa kwa hatifungani kwa wawekezaji wadogo wadogo. Toleo la kwanza lililofanywa na Benki ya Exim, ambapo jumla ya shilingi bilioni 19.97 zilikusanywa ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 10 na kupata wawekezaji 512. Hii inaonesha uhitaji uliokuwepo kwa wawekezaji wadogo wadogo katika fursa zinazopatikana katika uwekezaji wa hatifungani. Vile vile, Mamlaka iliidhinisha matumizi ya simu za mikononi kwenye ushiriki katika masoko ya mitaji kwa lengo la kuwawezesha Watanzania waishio vijiji na mijini kushiriki katika uuzaaji na ununuzi wa hisa, hatifungani za kampuni na vipande vyta uwekezaji wa pamoja kwa kutumia teknolojia hiyo.

101. **Mheshimiwa Spika**, maandalizi ya uanzishwaji wa Soko la Bidhaa (Commodity Exchange) nchini yamefikia hatua ya kuridhisha. Baadhi ya masuala ambayo yameshafanyika hadi sasa ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Masoko ya Bidhaa; Kuandaliwa kwa taratibu za ushiriki katika soko la bidhaa ambazo zitawezesha kutoa leseni na kuainisha taratibu za ushiriki katika Soko la Bidhaa la Tanzania; na kusajiliwa kwa Kampuni ya Soko la Bidhaa. Kufanikiwa kwa ukusanyaji wa mitaji na uorodheshwaji wa makampuni hayo kuliwezesha kuanzishwa kwa dirisha la kukuza ujasiriamali “Enterprise Growth Market” (EGM) katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Hadi Machi, 2016 makampuni matano yalikuwa yemeorodheshwa kwenye dirisha hilo.

(ii) **Soko la Hisa la Dar Es Salaam – DSE**

102. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kilichoishia Machi, 2016 Soko limeweza kuorodhesha Hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 783. Aidha, kwa upande wa hisa za makampuni, soko lilitorodhesha hisa milioni 61.8 zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 31. Idadi ya kampuni zilizoorodheshwa sokoni zimepanda mpaka kufikia kampuni 23 ikilinganishwa na kampuni 21 zilizokuwa zimeorodheshwa Julai, 2015.

Ongezeko hili limewezesha pia kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji kutoka 263,281 mwezi Julai 2015 hadi 464,000 mwezi Machi, 2016. Vile vile, katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi, 2016 hisa zenyenye thamani ya shilingi bilioni 632 ziliuzwa na hatifungani za Serikali zenyenye thamani ya shilingi bilioni 208 ziliuzwa katika soko la upili.

3.5.6. Dhamana za Uwekezaji Tanzania

(i) Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania - UTT MFI

103. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania (UTT MFI) imejikita katika kutoa huduma za kifedha na mikopo kwa watanzania wenyewe kipato cha chini na cha kati. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya mikopo ya shilingi bilioni 11.5 ilitolewa kwa wananchi 16,951 katil ya hao wanawake ni 13,561 na wanaume ni 3,390.

(ii) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji - UTT AMIS

104. ***Mheshimiwa Spika***, Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji na Huduma kwa Wawekezaji (UTT AMIS) ikiwa kama Meneja wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ilijikita zaidi katika kuimarisha, kuboresha na kukuza Mifuko mitano ya uwekezaji inayoisimamia ili iweze kutimiza malengo yake. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha, Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Jikimu na Mfuko wa Ukwasi. Hadi kufikia Machi, 2016 mifuko hii ilikuwa na jumla ya thamani ya shilingi bilioni 256 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 237 mwezi Disemba, 2015. Aidha, UTT AMIS iliendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia ya magazeti, redio na luninga kwa lengo la kuhamasisha tabia ya kujiwekea akiba na dhana nzima ya uwekezaji.

(iii) Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu - UTT PID

105. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu (UTT PID) imeweza kutekeleza majukumu yake yanayohusu kuibua na kutekeleza miradi kwa

kukamilisha upatikanaji wa viwanja vilivyopimwa kwa bei nafuu kwa wananchi katika sehemu za Sengerema, Mapinga, Kilwa, Lindi, Morogoro na Bukoba; kusaini makubaliano kati ya Taasisi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu uendelezaji wa viwanja vya balozi mbalimbali zilizopo nchi za nje; na kusaini mkataba wa kusimamia uendeshaji wa soko la kimataifa lililopo Mwanjelwa mkoani Mbeya. Aidha, Taasisi ipo katika hatua za awali za kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za mfano za askari wa Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT).

3.5.7. Taasisi za Mafunzo

(i) Chuo cha Usimamizi wa Fedha – IFM

106. ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Usimamizi wa Fedha- IFM kimeendelea kutoa mafunzo katika matawi yake yaliyoko Dar es Salaam na Mwanza katika fani za Usimamizi wa fedha, uhasibu, benki, bima, kodi, hifadhi za jamii, teknolojia ya mawasiliano ya habari, na sayansi ya komputa. Katika mwaka 2015/16, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 7,977 kati yao wanawake 3,042 sawa na asilimia 38.13 na wanaume 4935 sawa na asilimia 61.87. Aidha, wanafunzi 3,840 walihitimu masomo katika kozi mbalimbali.

(ii) Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini – IRDP

107. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa masomo 2015/16, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 4,622 katika kozi mbalimbali 17 zinazoendeshwa na Chuo. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, wanawake ni 2,362 sawa na asilimia 51 ya wanafunzi wote waliodahiliwa na wanaume ni 2,260 sawa na asilimia 49 ya wanafunzi waliodahiliwa. Aidha, Chuo kuitia Programu ya Kuboresha Elimu ya Msingi inayofadhiliwa na UKAID kimeendelea na uendeshaji mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kupanga na kusimamia mipango ya maendeleo ya sekta ya elimu ya msingi kwa Maafisa Elimu wa Wilaya katika mikoa saba ambayo ni Tabora, Dodoma, Simiyu, Shinyanga, Mara, Lindi, na Kigoma.

(iii) Taasisi ya Uhasibu Arusha – IAA

108. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2015/16, Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA) imeendelea kutoa elimu katika nyanja za uhasibu, ugavi, usimamizi wa kodi, benki, utawala wa biashara, teknolojia ya habari na sayansi ya kompyuta katika ngazi mbalimbali. Aidha, Chuo kinatoa mafunzo ya uhasibu na usimamizi wa fedha katika ngazi ya stashahada ya uzamili. Vilevile, Chuo kinatoa mafunzo ya shahada za uzamili (Masters Degree) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha “Coventry” cha Uingereza na Galgotias University, India. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: idadi ya wahitimu kuongezeka kutoka 1,367 mwaka 2014/15 mpaka 1,547 mwaka 2015/16. Hali kadhalika udahili wa wanafunzi uliongezeka kutoka wanafunzi 3,393 mwaka 2014/15 hadi wanafunzi 3645 mwaka 2015/16; Kuanza kutoa mafunzo katika Kampasi mpya ya Mwanza kwa ngazi ya Stashahada na Stashahada ya Uzamili; na kuanza kufundisha kwa kutumia mtandao ikiwa ni hatua muhimu ya kuanzisha kituo cha Elimu masafa (E-Learning Centre).

(iv) Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA

109. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) imeendelea kutoa mafunzo kuanzia ngazi ya cheti, diploma na shahada katika fani za uhasibu, uhasibu wa Serikali, ununuzi na ugavi, rasilimali watu, uongozi wa biashara, masoko na mahusiano ya umma kupitia matawi sita katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Singida, Mtwara, Mwanza na Kigoma. Katika mwaka wa masomo 2015/16, Taasisi ilidahili wanafunzi 7,473 katika kozi zake mbalimbali na hivyo kuifanya idadi ya wanachuo wote kufikia 14,758.

(v) Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika - EASTC

110. ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika, kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya uzamili, Shahada, Stashahada na Cheti cha

Takwimu Rasmi kwa nchi wanachama 18 ikiwemo Tanzania ambapo katika mwaka wa masomo 2015/16, jumla ya wanafunzi 421 walisajiliwa. Aidha, Chuo kilianza rasmi kozi ya Shahada ya Uzamili katika Takwimu za Kilimo kwa ushirikiano na Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) ambapo jumla ya wanafunzi watano walidahiliwa na kuanza masomo. Kadhalika, katika jitihada zake za kutambulika kimataifa katika kutoa huduma ya takwimu rasmi, kimeweza kupata hadhi ya kuwa Mwangalizi katika mikutano ya takwimu ngazi ya Umoja wa Mataifa (UN STACOM) kutohana na mchango wake katika ufundishaji wa takwimu rasmi kwa nchi zinazotumia lugha ya kiingereza barani Afrika.

3.5.8. Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo

(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA

111. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha mwaka 2015/16 Mamlaka ya Mapato Tanzania ilipanga kukusanya mapato ya kodi ya shilingi bilioni 12,362.96 ikiwa ni ongezeko la asilimia 24.8 ukilinganisha na makusanyo halisi katika mwaka wa fedha 2014/15. Kati ya kiasi kilichotarajiwa kukusanywa, shilingi bilioni 499.98 zilitarajiwa kupatikana kutohana na marekebisho ya mfumo wa kodi kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2015. Mapato ya kodi yalitarajiwa kuchangia asilimia 88 ya mapato ya ndani, wakati asilimia 12 iliyobaki ilitarajiwa kuchangiwa na mapato yasiyo ya kodi yakiwemo makusanyo ya Serikali za mitaa. Kwa upande wa Zanzibar, Mamlaka ya Mapato ilitarajiwa kukusanya mapato ya kodi ya shilingi bilioni 178.56 ikiwa ni ongezeko la asilimia 24 ukilinganisha na makusanyo halisi katika mwaka 2014/15. Hadi kufikia Machi, 2016 mapato halisi ya kodi kwa Tanzania Bara yalifika shilingi bilioni 9,251.87 sawa na asilimia 100.2 ukilinganisha na lengo la kukusanya shilingi bilioni 9,234.99 (**Jedwali Na.4**). Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 25.5 ukilinganisha na makusanyo yaliyofikiwa katika kipindi kama hiki katika mwaka wa fedha 2014/15.

112. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Zanzibar, hadi kufikia Machi, 2016 makusanyo halisi yalifika shilingi bilioni 121.1 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 132.25. (**Jedwali Na.5**). Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 91.5 ya lengo na ni

ongezeko la asilimia 13.3 ukilinganisha na makusanyo yaliyofikiwa katika kipindi cha mwaka 2014/15.

(ii) Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

113. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2015/16, Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu zilizohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Ofisi ya Taifa ya Takwimu imetayarisha na kusambaza takwimu za Pato la Taifa za robo ya pili, robo ya tatu na robo ya nne ya mwaka 2014 na sasa imekamilisha majumuisho ya takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka 2015. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa na takwimu mbalimbali zilizotokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 na kutoa machapisho yafuatayo: Taarifa za Vifo Nchini; Taarifa za Kazi na Ajira Nchini; Taarifa za Ndoa na Uzazi; Taarifa za Uhamiaji na Ukuaji wa Miji; Taarifa za Elimu na Kujua Kusoma na Kuandika; na Taarifa za Kijinsia.

114. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16 kazi ya uhakiki wa mipaka ya kiutawala zimekamilika katika maeneo ya Msitu wa Hifadhi ya Taifa wa Kazimzumbwi, Sikonge mkoani Tabora na Manyoni mkoani Singida. Vile vile uhakiki kwa wilaya za Gairo, Chemba na Wete zimekamilika. Kazi ya uhakiki wa mipaka ya kiutawala inafanyika kwa lengo la kuboresha kanza ya kijiografia inayotokana na Sensa ya Watu na Makazi. Aidha, kazi ya kuhakiki mipaka ya utawala katika ngazi ya vijiji na mitaa imefanyika katika wilaya za Bagamoyo kwa mkoa wa Pwani na Kiteto katika mkoa wa Manyara. Kazi hii inalenga maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

(iii) Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha – SELF Microfinance Fund

115. ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa SELF ambao ni mwendelezo wa mradi wa SELF uliofikia ukomo wake Juni, 2015 unalenga kukuza na kupanua upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wananchi hususani wa vijijini. Mfuko huu kwa kushirikiana na asasi 59 umeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali ambapo hadi kufikia Machi, 2016, mikopo yenyе thamani ya shilingi bilioni 5.76 ilikopeshwa kwa wajasiriamali wadogo wadogo 4,189 kati yao 2,279 (asilimia 54.4) ni wanawake na wanaume ni 1,910 (asilimia 45.6). Mikopo ililenga maeneo mbalimbali ikiwemo mikopo ya biashara ndogo ndogo, ufgaji, uvuvi, usindikaji, madini, viwanda vodogo vidogo, huduma mbalimbali za kibiashara pamoja na pembejeo za kilimo. Aidha, urejeshaji wa mikopo katika Mfuko wa SELF umefikia kiwango cha asilimia 90.

(iv) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi – NBAA

116. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi imeendelea kusimamia matumizi ya viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za fedha katika Serikali Kuu na Idara zake, Sekta Binafsi pamoja na Mashirika Binafsi (NGOs). Hadi Machi, 2016 Bodi ilitekeleza majukumu yafuatayo:- Kusimamia utumiaji wa viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za hesabu nchini; kuhariri mitaala pamoja na silabi ya taaluma ya uhasibu; kuendeleza taaluma ya uhasibu; kufanya usajili wa wahasibu na kutunza takwimu; pamoja na kusimamia ubora wa ukaguzi wa hesabu.

(v) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha - Gaming Board

117. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, Bodi iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuratibu sekta ya michezo ya kubahatisha nchini. Katika kutekeleza majukumu hayo, Bodi iliendelea kutoa leseni mbalimbali za michezo ya kubahatisha. Aidha, katika kipindi hicho Bodi ilifanya kaguzi za mara kwa mara kwa

waendeshaji wa michezo ya kubahatisha nchini ili kuhakikisha kuwa michezo hiyo inaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya michezo hiyo pamoja na sheria zingine za nchi.

118. **Mheshimiwa Spika**, Bodi pia iliendelea kukusanya kodi itokanayo na michezo ya kubahatisha nchini; yaani “gaming tax”. Hadi kufikia Machi, 2016 makusanyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 18.19, sawa na asilimia 86 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 19.01. Makusanyo ya mwaka 2015/16 yanatarajiwu kukua kwa asilimia 79 ikilinganishwa na mwaka 2014/15. Aidha, Bodi inatarajia kuchangia kiasi cha shilingi bilioni 1.44 katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria. Hii ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 95 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi milioni 734.39 zilizopelekwa mfuko Mkuu wa Serikali mwaka 2014/15.

3.5.9. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Mwaka 2015/16

119. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2015/16, Wizara ilipanga kutekeleza miradi ifuatayo: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Ujenzi wa Kituo cha Elimu cha Uhasibu; Ujenzi wa Maktaba ya Kisasa ya Chuo cha Uhasibu Arusha; Kujenga uwezo wa kiutendaji kwa Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Mikoa; Maboresho ya Usimamizi wa Kodi; Mpango Kabambe wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania; Uwezeshaji wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi; Mradi wa Uwezeshaji Wajasiriamali Wadogo; Mpango wa Taifa wa Kuongeza Kipato; na Mpango Kabambe wa Kutathmini Umaskini (Poverty Monitoring Master Plan).

120. **Mheshimiwa Spika**, Miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na: Social Policy Analysis and Development; Pro-Poor Growth; Uratibu wa Miradi ya Maendeleo; na Population Planning.

121. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi, 2016 miradi iliyopata fedha ni miwili tu ambayo ni: Programu ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) na Mpango Kabambe

wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania (TSMP). Shughuli zilizofanyika chini ya mradi wa PFMRP ni pamoja na: kufanya tathmini ya mafunzo yaliyoendeshwa chini ya programu ya maboresho kwa kipindi cha mwaka 2012/13 hadi 2014/15; kufanya tathmini ya utekelezaji wa programu ya PFMRP kwa kipindi cha miaka miwili na nusu ya utekelezaji; kuendesha mafunzo ya result based management kwa maafisa 63 kutoka Ofisi mbalimbali za Serikali; kutekeleza mpango kazi wa kuwianisha mifumo ya usimamizi wa fedha;

122. ***Mheshimiwa Spika***, shughuli nyingine zilizotekelawa chini ya programu hii ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wakaguzi 74 juu ya namna ya kutumia software kufuatilia hoja za kiukaguzi zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambazo hazijafanyiwa kazi; kukamilisha uandaaji wa Sera ya Usimamizi wa Mali ya Serikali; ufuatiliaji wa Kamati za Ukaguzi 60 katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Mikoa ili kuhakikisha zinazingatia miongozo ya ukaguzi; Kuwajengea uwezo Wakuu wa Idara 50 kutoka kwenye Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa vihatarishi; na kuhakiki na kuhuisha kanzidata ya taarifa za watumishi wa kada za ununuzi na ugavi katika mikoa ya Geita, Katavi, Manyara, Njombe na Simiyu.

123. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mpango Kabambe wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania (TSMP), shughuli zilizofanyika ni pamoja na: kufanya utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Utafiti wa Viashiria vya Malaria wa 2015/16 (Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey); Kufanya Utafiti na kutoa Matokeo ya Tathmini ya Utoaji wa Huduma za Afya Tanzania, 2014/15 (Tanzania Service Provision Assessment Survey 2014-15; na kufanya utafiti wa kufuatilia hali ya umaskini katika Kaya (National Panel Survey) wa mwaka 2014/15.

3.6. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI

3.6.1 MAFANIKIO

124. ***Mheshimiwa Spika***, Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/16 ni pamoja na: Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani; Kuendelea kutengemaa na kukua kwa uchumi kwa asilimia 7.0 mwaka 2015; Kuendelea kupungua kwa mfumuko wa bei na kufikia asilimia 5.4 Machi, 2016; Utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuitia mapato ya ndani kama vile usambazaji wa umeme vijijini, Kinyerezi II pamoja na miradi ya umeme yenyeye vyanzo vyta mapato ikijumuisha mfuko wa barabara, mfuko wa maji vijijini na Mamlaka ya Elimu; Kufanikisha uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kwa kutumia fedha za ndani; Kupunguza malimbikizo ya madai ya watumishi, wazabuni na wakandarasi yaliyohakikiwa; Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu; na Kuanza utekelezaji wa elimu msingi bila malipo kwa kutenga shilingi bilioni 18.8 kila mwezi.

3.6.2 CHANGAMOTO

125. ***Mheshimiwa Spika***, panapo mafanikio, changamoto nazo hazikosekani. Hivyo, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/16 ulikabiliwa na changamoto za ukwepaji wa kodi unaohusisha wafanyabiasha na watumishi wasio waadilifu; Mwitikio hasi kwenye matumizi ya mashine ya kielektroniki (EFDs); Ukwepaji kodi kwa kampuni za kimataifa unaotokana na na kampuni hizo kutumia bei kubwa kuliko za soko kwenye biashara baina ya kampuni tanzu na kampuni mama (Transfer Pricing); Uwepo wa sekta kubwa isiyo rasmi ambayo hailipi kodi; na Kuwepo kwa taasisi nyingi zinazokusanya maduhuli kunakosababisha kuwa na idadi kubwa ya kodi zinazolalamikiwa na wafanya biashara.

126. ***Mheshimiwa Spika***, changamoto nyingine ni pamoja na uwepo wa malalamiko ya utozaji kodi mara mbili kwa bidhaa zinazopitia Zanzibar kutokana na mfumo wa

mgawanyo wa mapato unaopelekea kuwa na mifumo tofauti ya ukokotoaji kodi kwa bidhaa zinapoingia Zanzibar; Uvujaji wa mapato kutokana na kuwa na sheria ambazo hazijalenga zaidi mienendo ya biashara za sekta mpya kama mafuta na gesi; Kuwepo kwa bandari bubu na njia za panya zinazoingiza bidhaa nchini bila kulipiwa kodi. Kupungua kwa fedha za misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo kutokana na kuibuka kwa masharti mapya yanayoambatana na utoaji wa fedha hizo nje ya makubaliano ya awali; na ufanisi duni wa baadhi ya mashirika (kama vile ATCL, TRL, na TAZARA) unaolazimu kuendelea kupata ruzuku ya mishahara na uendeshaji kutoka Serikalini.

3.6.3 HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

127. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa bajeti kama zilivyobainishwa hapo juu, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo: Kusimamia dhana ya kulipa kodi kwa hiari kwa wafanyabiashara na uwajibikaji kwa watumishi wasio waadilifu; Kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu na faida za kulipa kodi kwa kutumia mitandao ya kielektroniki; na Kuendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za kurasimisha shughuli za sekta isiyo rasmi ikiwa ni pamoja na kufanya uthamini wa mkupuo wa majengo ili kufanikisha ukusanyaji wa kodi ya majengo.

128. ***Mheshimiwa Spika***, hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuboresha Sheria ya Kodi (2004) kwa kuanzisha sheria ya kodi inayojitegemea ambayo itasimamia shughuli za uchimbaji madini, gesi na mafuta; Mamlaka ya Mapato Tanzania kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kupambana na biashara za bandari bubu na njia za panya; Kuendelea na majadiliano baina ya Serikali na Wahisani ili kuhakikisha kwamba fedha za misaada na mikopo zinapatikana kama ilivyoahidiwa na kwa wakati; na Serikali inakusudia kufanya marekebisho makubwa kwa Mashirika ya Umma ili yaweze kujiendetsha kibiashara bila kutegemea ruzuku ya Serikali.

4.0 MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17

129. ***Mheshimiwa Spika***, Baada ya kuelezea utekelezaji wa mjukumu ya Wizara kwa kina kwa mwaka 2015/2016, naomba sasa nieleze malengo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2016/17.

4.1 MAJUKUMU YA WIZARA

4.1.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

130. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kuendelea kuimarisha Sera ya fedha ili iendane na sera ya bajeti kwa lengo la kudhibiti na kupunguza mfumuko wa bei pamoja na tofauti kati ya riba za amana na zile za mikopo.

4.1.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa

131. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Wizara chini ya uratibu wa mipango ya maendeleo imepanga kuendelea kuwaelimisha wadau mbalimbali kuhusu wajibu wao katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2020/21); Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18; Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na; Kuchapisha, kusambambaza na kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (PIM – OM). Shughuli hii inalenga kuimarisha taratibu za uibuaji, utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa miradi inayoibuliwa inatekelezwa kikamilifu na kwa mafanikio makubwa.

4.1.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini

132. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa mwaka 2016/17 imepanga kuandaa mpango wa kitaifa wa ufuatiliaji na tathmini wa jitihada za kuondoa umaskini, ikiwemo viashiria vya kupima utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mpango huu utasaidia kufuatilia utekelezaji wa programu za kuondoa umaskini katika sekta mbalimbali, kuibua changamoto na kurekebisha kasoro kila mwaka; Kuandaa taarifa ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu; Kuanzisha kituo cha utunzaji na utoaji wa taarifa mbalimbali kuhusu programu za kuondoa umaskini na maendeleo ya watu; Kuandaa mwongozo wa namna ya kuibua na kutumia fursa za kiuchumi katika maeneo yanayowazunguka wananchi katika halmashauri mbalimbali nchini. Hatua hii itaongeza ushiriki wa wananchi hususani vijijini katika miradi ya uzalishaji na kuongeza kipato; na kufanya tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya kuondoa umaskini hususan namna bora na endelevu ya kuboresha jitihada za Serikali katika kuinua hali ya maisha ya watanzania walio chini ya mstari wa umaskini na kuongeza kasi katika kuleta maendeleo ya binadamu.

4.1.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

(a) Mapato ya Ndani

133. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato, katika mwaka 2016/17 Wizara pamoja na mambo mengine imepanga kuendelea na mfumo wa dirisha moja la kielektroniki kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Mapato; kuendelea kudhibiti mizigo yote inayoingia kutoka bandari kavu zote; kuendelea kuimarisha mapato kwenye ushuru wa forodha na bidhaa; kuendelea kusimamia matumizi ya mashine za kielektroniki (EFDs); kushughulikia kwa haraka rufaa za pingamizi na kodi; kufanya kaguzi kwa kuzingatia viashiria hatarishi vya uvujaji wa mapato ya Serikali; kusimamia misamaha ya kodi ili kuhakikisha inatolewa tu kwa wale wanaostahili na

inatumika ipasavyo na; kuendelea kutoa elimu ya walipa kodi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi.

(b) Misaada na Mikopo

134. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2016/17 Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kupata fedha za nje za kugharamia miradi ya maendeleo. Serikali itaelekeza fedha za nje katika kutelekeza miradi mikubwa ya maendeleo itakayochocha ukuaji wa uchumi sambamba na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya Serikali. Hata hivyo, azma ya Serikali ni kupunguza na hatimaye kuondokana na utegemezi wa kibajeti.

135. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo tumekubaliana kuwaleta Washauri Elekezi wa kimataifa ili waweze kufanya tathmini ya ushirikiano wetu pamoja na namna ya kuendesha majadiliano. Lengo ni kuboresha ushirikiano wa maendeleo na kushauriana na Serikali juu ya njia nzuri ya kupokea fedha za nje ili ziweze kuwekezwa kwenye miradi ya maendeleo yenye kuleta ufanisi zaidi.

4.1.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

136. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa mwaka 2016/17 imepanga pamoja na mambo mengine kuendelea kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali inayojumuisha matumizi ya kawaida na maendeleo; Kuendelea kupitia mfumo wa uwasilishaji wa bajeti za Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri na kuhakikisha kuwa Sera na Mipango ya Kitaifa na ile ya Kisekta vyote vimeingizwa ipasavyo katika Bajeti ya Serikali na kutengewa fedha; Kufanya tathmini ya Bajeti ya Serikali kwa lengo la kuhakikisha kuwa inazingatia mahitaji ya makundi yote ya jamii; Kuendelea kuimarisha mifumo ya Kompyuta ya uandaaji bajeti ili kukidhi mahitaji ya

taarifa mbalimbali zinazohitajika na; Kuendelea kujenga uwezo wa Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Idara katika uandaaji wa bajeti ya muda wa kati, usimamiaji wake na utoaji taarifa za utekelezaji ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji na tathmini kwa wakati.

4.1.6 Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma

137. ***Mheshimiwa spika***, katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kuandaa na kukamilisha Mpango wa Programu wa Awamu ya Tano wa Miaka Mitano 2017/2018 - 2021/22; Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Serikali wa kada zinazohusiana na usimamizi wa fedha za umma; Kufanya tathmini ya utekelezaji wa programu kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ili kupima mafanikio ya utekelezaji wa Progam ya Awamu ya Nne na; Kusimamia na Kuratibu zoezi la Upimaji wa Mifumo ya Fedha - *Public Expenditure and Financial Accountability* katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

4.1.7 Usimamizi wa Malipo

138. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kuendelea kutoa udhamini wa masomo kwa wahasibu, wakaguzi, wagavi na wataalamu wa kompyuta kutoka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ambao wapo vyuoni; Kusimika Mfumo wa TISS katika Halmashauri zipatazo 58 zilizopo katika Mikoa ya Dar es salaam, Mbeya, Mwanza, Arusha, Tanga, Morogoro na Dodoma. Wizara imepanga kuendelea kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na uunganishaji wa mtandao wa malipo wa Serikali. Aidha, Wizara imepanga kuunganisha Mfumo wa Malipo wa EFT katika Wizara ya Fedha na Mipango, Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii; Kuunganisha mfumo wa uwasilishaji mapato wa Mamlaka ya mapato Tanzania - Tanzania Revenue Gateway System (RGS) na mfumo wa Hazina - Treasury Revenue Accounting System kwa lengo la kupata taarifa za mapato ya kodi kutoka TRA kielektroniki.

139. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imepanga pia kufuatilia utekelezaji wa Miongozo ya ukaguzi wa ndani; kukagua mfumo wa kuandaa bajeti; Kufanya ukaguzi maalum kadri ya mahitaji ya Mlipaji Mkuu wa Serikali na wadau wengine; na kuendelea kutoa mafunzo na kufanya ufuatiliaji wa miongozo mbalimbali ambayo imetolewa na Wizara kwa wakaguzi wa ndani wote na wadau mbalimbali wanaotumia miongozo hiyo.

4.1.8 Deni la Taifa

140. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa mwaka 2016/17 imepanga kuendelea kulipa madeni mbalimbali yaliyokopwa na Serikali ili kugharamia miradi ya maendeleo nchini pamoja na kuwasilisha michango ya Serikali kwenye mifuko ya hifadhi za jamii. Aidha, kwa kuwa malipo ya fidia kwa wafanyakazi waliokuwa wakipata ajali mahala pa kazi yalikuwa hayashughulikiwi ipasavyo na waajiri na mifuko iliyopo ya Hifadhi ya Jamii ambayo mingi ni ya Pensheni, Serikali ilianzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na Wizara kwa mwaka 2016/17 imepanga kuanza kuwasilisha mchango wa mwajiri kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ili watumishi wa umma wakipata ajali mahala pa kazi waweze kulipwa na Mfuko huu kwa wakati na pia kupata malipo yenyе staha.

4.1.9 Usimamizi wa Mali ya Serikali

141. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Wizara chini ya jukumu lake la kusimamia mali ya Serikali imepanga kufanya uthamini wa ardhi na majengo ili kuwa na taarifa sahihi za mali ya Serikali; Kuendelea kuondosha mali chakavu, sinzia na zilizokwisha muda wake; na Kufanya uhakiki wa mali za watu binafsi zilizo chini ya uangalizi wa Serikali na zile zinazotokana na utaifishwaji kwa lengo la kuepuka ulipaji wa fidia usiokuwa wa lazima. Aidha, Wizara itahakiki mali katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali ili kutoa ushauri wa kupunguza hasara zinazotokana na matumizi yasiyo sahihi.

4.1.10 Ununuzi wa Umma

142. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: Kufanya mapitio ya kanuni za ununuzi wa umma; Kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi wa umma nchini; Kuwajengea uwezo wadau mbalimbali wa ununuzi nchini juu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma na kukamilisha tathmini ya ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa umma nchini. Aidha, Wizara imepanga kutekeleza mpango wa mahitaji ya mafunzo wa maafisa ununuzi na ugavi walioko katika Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuwajengea uwezo juu ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi; Kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa malipo wa EPICOR 9 kwa baadhi ya maafisa ununuzi na ugavi Serikalini pamoja na kuendelea kuhakiki taarifa za maafisa ununuzi na ugavi na kuziweka katika daftari la maafisa ununuzi na ugavi Serikalini.

143. **Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizopangwa kufanywa na Wizara kwa mwaka 2016/17 ni pamoja na kukamilisha mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao na kuanza kuutumia kwa majoribio kwenye robo ya pili ya mwaka 2016/17 kwa manunuzi ya madawa na vifaa tiba pamoja na manunuzi ya bidhaa mtambuka; Kuongeza uwezo wa watumiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa kufanya mafunzo kwa wanataaluma na wadau wengine ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti juu ya taaluma ya ununuzi na ugavi utakaopelekea kutoa ushauri kwa Serikali kwenye maeneo ya taratibu na sera za ununuzi na ugavi na; Kuongeza kiwango cha ufaulu wa watahiniwa toka kiwango cha sasa cha asilimia 42.8 hadi kufikia asilimia 50 kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia.

144. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kuitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini imepanga kuendelea na ununuzi wa magari kwa pamoja; Kuongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi mafuta kufikia wastani wa litu 50,000 kila mkoa katika mikoa ya Iringa, Kigoma, Mbeya, Morogoro na Mwanza; Kuanza ujenzi wa ofisi, ghalbali na kisima cha mafuta katika mikoa ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu. Aidha, Wakala

wa Huduma ya Ununuzi Serikalini utaendelea na kazi ya kufunga mfumo wa udhibiti na usimamizi wa mafuta ya magari na mitambo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mwanza, Morogoro, Ruvuma, Singida na Tanga.

4.1.11 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

145. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imelenga kuendelea kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2015/16. Ukaguzi utaelekezwa katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma. Aidha, ukaguzi utahusisha Sekta ya mafuta na gesi na pia ukaguzi katika sekta ya madini utaimarishwa ipasavyo. Wizara itaendelea kuimarishe uwezo wa kitaalam kwa Wakaguzi wake, na kuendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ili kuimarishe uhuru wa wakaguzi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija zaidi ili kukidhi matakwa ya viwango vya kimataifa vya taasisi za ukaguzi pamoja na maazimio ya kimataifa ya Lima na Mexico ambayo Tanzania imeyaridhia.

4.1.12 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma

146. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Wizara kupitia Msajili wa Hazina, itaendelea kufanya uhakiki wa mali za taasisi na mashirika za umma zilizoingizwa katika daftari la mali; Kufuatilia na kuhakiki mali za mashirika yaliyobinafsishwa ili kubaini mali ambazo hazikuingizwa kwenye orodha ambazo hivi sasa zinamilikiwa kinyume na sheria ili zirejeshwe Serikalini; Kufanya utafiti wa taasisi ambazo zina vyanzo binafsi vya mapato kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kuziondoa kwenye utegemezi wa ruzuku ya Serikali; na kukamilisha maandalizi ya mfumo wa tathmini na ufuutiliaji kwa taasisi na mashirika ya umma.

4.1.13 Mafao ya Wastaafu na Mirathi

147. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016/17 shilingi trilioni 1.14 zimetengwa kwa ajili ya kulipa mchango wa mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha kumbukumbu za wastaafu ikiwa ni pamoja na kulipa pensheni kwa wakati.

4.1.14 Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi

148. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi; Kuendelea kuwasilisha taarifa za intelijensia kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi; Kukamilisha zoezi la kutathmini mianya na viashiria vya fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi nchini; Kuendelea na utekelezaji wa mikakati ya kitaifa na kimataifa ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi; na kuendelea na ukaguzi wa taasisi mbalimbali za fedha na zisizo za fedha ili kubaini kama sheria na miongozo ya kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu na ufadhilli ugaidi inafuatwa ipasavyo.

4.1.15 Tume ya Pamoja ya Fedha

149. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016/17 Wizara kuitia Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kuendelea kufanya stadi ya uwekezaji katika mambo ya muungano. Stadi hii inalenga kubaini ushiriki wa pande mbili za muungano katika uwekezaji kwa mambo ya muungano. Aidha, Wizara inakusudia kufanya mapitio ya stadi zilizofanywa na Tume kuhusu mfumo bora wa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa masuala ya fedha yanayohusu mambo ya muungano.

4.1.16 Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi

150. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Wizara itaendelea kupokea na kuchambua miradi ya ubia kwa lengo la kuiidhinisha; Kutoa ushauri kwa Wizara na Taasisi za Serikali katika kuchagua miradi bora ya ubia; Kuziwezesha taasisi zenyenye miradi ya ubia kuajiri washauri elekezi pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu sera, sheria na kanuni za miradi ya ubia.

4.2 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA

4.2.1 Huduma za Kibenki

(i) Benki Kuu ya Tanzania – BoT

151. ***Mheshimiwa Spika***, ili kufikia malengo ya uchumi mpana ambayo Serikali imojiwekea, Benki Kuu ya Tanzania katika mwaka wa fedha 2016/17 imeweka malengo yafuatayo:- Ukuaji wa wastani wa fedha taslim usiozidi asilimia 13; Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsirsi pana zaidi wa asilimia 14.8; Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 20.5; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.

(ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo -TADB

152. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016/17, Benki imepanga kuendelea kutoa mikopo kwa angalau minyororo 14 ya thamani (agricultural value chains) itakayofanyiwa tathmini yakinifu kama iliyohanishwa kwenye mpango kazi wa kwanza wa 2016-2020; Kufanya maandalizi ya kutoa mikopo ya kuendeleza miradi ya Kilimo cha umwagiliaji; Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Benki, mabenki mengine na wadau mbali mbali wa Kilimo hususan wale watakaoshiriki katika hatua mbalimbali za mchakato wa kutoa mikopo; Kuitangaza benki na huduma zake kwa wananchi ili

waweze kuzielewa shughuli zake na jinsi benki itakavyowahudumia; Kufungua Ofisi za kikanda katika kanda sita katika Kipindi cha miaka mitano ya kwanza kulingana na ukuaji wa biashara na upanuzi wa huduma mikoani; Kusimamia utoaji na usimamizi wa fedha kwenye uendeshaji wa miradi ya Kilimo mbalimbali nchini; na kuratibu upatikanaji wa dhamana mbalimbali kwa ajili ya mikopo kwa wakulima ili mabenki yaweze kuelekeza nguvu zao kuwakopesha wakulima wengi zaidi.

(iii) Benki ya Maendeleo TIB – TIB DFI

153. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016/17 Benki ya Maendeleo TIB imepanga kuongeza utoaji mikopo katika sekta mbalimbali hadi kufikia shilingi bilioni 726.9, kutoka shilingi bilioni 538.7 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 35; Waraka mizania unategemewa kukua kufikia shilingi bilioni 872.2 Disemba, 2016, kutoka shilingi bilioni 689.0 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 27. Faida kabla ya kodi inategemea kufikia shilingi bilioni 13.1 ifikapo Disemba, 2016, kutoka shilingi bilioni 9.2 Disemba, 2015 ambalo ni ongezeko la asilimia 42. Aidha, Ili kugharimia ukuaji huo, benki imepanga kukopa fedha za muda mrefu na wa kati kufikia shilingi bilioni 325.0 ikijumuisha shilingi bilioni 100 zinazotazamiwa kutohana na Hati Fungani (Corporate Bond). Benki imepanga kukusanya amana za wateja kufikia shilingi bilioni 301.5 mwaka 2016/17.

(iv) Benki ya Biashara TIB – TIB CBL

154. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016/17 Benki ya Biashara TIB imepanga kuongeza utoaji mikopo ya muda mfupi na wa kati kama mitaji ya uwendeshaji (working capital) katika sekta mbalimbali hadi kufikia shilingi bilioni 176.5, kutoka shilingi bilioni 114.4 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 54.3; Waraka mizania unategemewa kukua kufikia shilingi bilioni 348.8 Disemba, 2016, kutoka shilingi bilioni 219.1 Disemba, 2015 sawa na ongezeko la asilimia 59.2. Faida kabla ya kodi inategemea kufikia shilingi bilioni 8.8 ifikapo Disemba, 2016 kutoka shilingi bilioni 5.3

Disemba, 2015 ambalo ni ongezeko la asilimia 70. Aidha, Ili kugharimia ukuaji huo, benki ya TIB CBL imepanga kukusanya amana za wateja kufikia shilingi bilioni 298.0 kwa mwaka 2016.

(v) Benki ya Posta Tanzania – TPB

155. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016, Benki imejipanga kufikia malengo yafuatayo kibiashara; Kuongeza mapato ya Benki na kufikia shilingi bilioni 89.1; Kupata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 12.6; Kukuza amana za benki na kufikia shilingi bilioni 382.59; Kuongeza thamani ya mikopo hususan kwa wananchi wa kipato cha chini na kufikia shilingi bilioni 334.504; Kukuza thamani ya mtaji mpaka kufikia shilingi bilioni 51.1; na kuongeza idadi ya wateja wapya wa benki hadi kufikia wateja milioni moja na laki moja.

(vi) Twiga Bancorp

156. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016, benki imeweka lengo la kukusanya na kukuza amana za wateja kufikia shilingi bilioni 146.9 kutoka shilingi bilioni 86.3 za Disemba, 2015 hii ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 60.6 au asilimia 71. Aidha, kutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara benki inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 14.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11.2 zilizokusanywa mwaka 2015, hii ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 3.5 au asilimia 31 ikilingnishwa na mapato yaliyokusanywa mwaka wa 2015.

157. ***Mheshimiwa Spika***, benki kwa kushirikiana na mawakala wa ukusanyaji madeni imejiweka lengo la kukusanya madeni ya shilingi bilioni tano kutoka kwa wateja wa mikopo ambao wamekuwa sugu. Aidha, benki imejiwekea lengo la kutoa mikopo kwa

wateja mbalimbali itakayofikia shilingi bilioni 70 kutoka shilingi bilioni 37.4 ilivyokuwa Disemba, 2015 hii ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 32.6 au asilimia 88.

158. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa uwekezaji, benki imeweka lengo la kuwekeza kiasi cha shilingi bilioni 61.6 katika Dhamana za Serikali na Amana za muda maalumu kwenye mabenki ikilinganishwa na Dhamana pamoja na Amana zenyet thamani ya shilingi bilioni 39 zilizowekezwa hadi Disemba, 2015. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 22.6 au asilimia 58.

4.2.2 Mfuko ya Hifadhi za Jamii

(i) Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma – PSPF

159. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2016/17 Mfuko unatarajia kusajili wanachama 30,000 na kuongeza idadi ya wanachama hadi kufikia 476,190 Juni, 2017. Aidha, Mfuko unatarajia kukusanya shilingi bilioni 803.22 kutokana na michango ya wanachama, shilingi bilioni 90.48 mapato kutokana na vitega uchumi mbalimbali, shilingi bilioni 510.92 kutokana na vitega uchumi viliyvo komaa na shilingi bilioni 173.64 kutokana na deni la michango kwa Serikali kabla ya Julai, 1999. Mfuko unatarajia kuwekeza shilingi bilioni 554.40 kwenye vitega uchumi, shilingi bilioni 1,040.15 zitatumika kulipa mafao, shilingi bilioni 2.99 zitalipwa kwa SSRA kama ada ya mwaka na shilingi bilioni 49.07 zitakuwa gharama za uendeshaji. Mafanikio ya malengo haya yataongeza thamani ya Mfuko kutoka shilingi trilioni 1.46 zinazokadirwa mwezi Juni, 2016 hadi kufikia shilingi trilioni 1.55 ifikapo Juni, 2017.

(ii) Mfuko wa Mafao ya Kustaafu – GEPF

160. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Mfuko utaendelea na jitihada zake za kupanua wigo wa wanachama na hivyo kusajili wanachama zaidi kuitia mpango wa hiari wa kuiwekea akiba ya uzeeni na mpango wa lazima. Mfuko pia utaboresha

huduma kwa wanachama kwa kuwekeza zaidi katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, kukuza mapato yatokanayo na uwekezaji kwa kuwekeza katika maeneo salama na yenye kuleta mapato zaidi. Hadi kufikia Juni, 2017 Mfuko unatarajia kusajili jumla ya wanachama 33,007 na kukusanya michango yenye thamani ya shilingi bilioni 81.64. Kadhalika, mapato yatokanayo na uwekezaji yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia Shilingi bilioni 56.90 ifikapo Juni, 2017. Thamani ya Mfuko hadi kufikia Juni, 2017 inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 697,217.72.

(iii) Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma – PPF

161. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha mwaka 2016/17, thamani ya Mfuko inategemea kukua hadi kufikia shilingi trilioni 2.9. Ukuaji huu utatokana na kufikiwa kwa malengo yatakayowekwa katika kukusanya michango kutoka kwa wanachama ya kiasi cha shilingi bilioni 420, kuongezeka kwa uwekezaji utakaoupatia Mfuko mapato yatakayotokana na uwekezaji yanayotarajiwa kufikia shilingi bilioni 260 ifikapo Juni, 2017. Aidha, katika mwaka 2016/17, Mfuko unategemea kuandikisha jumla ya wanachama wapya 66,660 kutoka katika sekta ya umma na binafsi.

4.2.3 Rufani za Kodi

162. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi na Baraza kwa mwaka 2016/17 zitaendelea kusikiliza na kutolea maamuzi rufaa za kodi zitakazowasilishwa ili kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa wakati.

4.2.4 Huduma za Bima

(i) Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima – TIRA

163. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016/17, Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imepanga kuanza kutekeleza Sera mpya ya Bima. Sera hii itafungua milango ya uwekaji bima za kilimo na mifugo, bima kwa ajili ya watu wa kipato cha chini ikiwa ni

pamoja na kupata huduma za bima kuitia mabenki. Lengo ni kuongeza mchango wa Bima kwenye pato la Taifa kutoka asilimi 0.9 za sasa hadi asilimia 3 ifikapo mwaka 2019.

164. ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka imepanga pia kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Elimu ya Bima kwa Umma kwa lengo la kuhakikisha ifikapo mwaka 2017 asilimia 25 ya Watanzania wote wawe wamefikiwa na huduma za bima. Aidha, Mamlaka kwa mwaka 2016/17 imepanga kufanya marejeo ya Sheria ya Bima, Namba 10 ya 2009 ili kuvutia uwekezaji mkubwa katika biashara ya bima wenyewe lengo la kukidhi mahitaji ya sasa ya soko la bima ndani ya nchi hususan bima za gesi na mafuta.

(ii) Shirika la Bima la Taifa – NIC

165. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Shirika litaendelea na mkakati wa kujitangaza zaidi ili kuongeza biashara kwa kubuni bima mpya zitakazokidhi mahitaji ya wananchi, ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia ya mawasiliano kuitia mitandao ya simu za mkononi. Shirika pia litaendelea kutoa elimu ya bima kwa wananchi kuitia njia mbalimbali, kwa mfano redio, luninga na vipeperushi. Pia kukamilisha mipango yote kama ilivyoainishwa kwenye Mpango Mkakati wa Shirika.

4.2.5 Mitaji na Dhamana

(i) Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana – CMSA

166. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Mamlaka ya Masoko na Mitaji imepanga kutayarisha Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Maendeleo ya Masoko ya Mitaji (National Capital Market Master Plan); Kukamilisha hatua za kuanzishwa kwa biashara katika Soko la Bidhaa (Tanzania Mercantile Exchange -TMX) ambalo litaanzishwa kwa ubia wa sekta ya umma na binafsi; Kuendelea kuboresha uongozi wa Soko la Hisa la Dar es Salaam ili kulifanya soko lijiendeshe kibiashara (Exchange Demutualization) na

kuondokana na utegemezi kwa Serikali; Kuanzisha misingi ya kusimamia masoko kwa kuzingatia uzito wa athari (risk based supervision) ambapo mahitaji tofauti yatabainishwa kwa taasisi tofauti kulingana na kazi zao; na Kuendelea kushawishi kampuni za umma zinazofanya vizuri kuorodhesha hisa zake katika soko la hisa.

(ii) Soko la Hisa la Dar Es Salaam – DSE

167. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016/17, Soko la Hisa la Dar Es Salaam limepanga kuongeza idadi ya kampuni katika Soko la Hisa kwa ushawishi na kuzishauri Serikali na sekta binafsi kuuza hisa zao kupitia soko la hisa; Kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali kuweka mazingira yatakayowezesha kampuni za sekta muhimu kama madini na mawasiliano ya simu kuorodhesha sokoni; Kuanzisha aina mpya za Dhamana za muda mrefu kama hatifungani za Serikali za mitaa na miundo mbinu; Kuongeza ufanisi wa shughuli za minada kwa njia ya simu na mtandao wa intaneti; Kuendelea na juhudhi mbalimbali zinazolenga kuongeza ufahamu wa masuala ya masoko ya mitaji kwa umma; na Kuendelea kutoa nafasi kwa wajasiriamali wadogo na wa-kati ili waweze kunufaika na dirisha dogo la DSE la EGM katika kufanikisha malengo yao ya kuanzisha biashara au kuendeleza biashara.

4.2.6 Dhamana za Uwekezaji Tanzania

(i) Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania - UTT MFI

168. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania inatarajia kutoa mikopo kwa wafanyakazi wa umma, wafanyabiashara, na wakulima wapatao 64,715 yenye thamani jumla ya shilingi 43,000,000,000; Kuomba leseni ya kupokea akiba toka kwa wanachama kutoka Benki Kuu ili kupata mtaji wa kujiendesha na kutoa mikopo yenye gharama nafuu kwa watanzania walio na kipato cha chini; na kufungua matawi mengine manne ili kuwafikishia huduma wananchi wengi zaidi.

(ii) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji - UTT AMIS

169. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji itaendelea na jitihada za kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Mifuko ili kuongeza thamani ya Mifuko na ukuaji wa thamani kwa kila kipande kinachowekezwa. Aidha, kampuni pia itafanya jitihada za kutoa elimu kwa umma ili wananchi waelewe fursa zinazotolewa na mifuko ya uwekezaji wa pamoja na kufanya jitihada ili kuwafikia watanzania wengi zaidi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili waweze kupata huduma zinazotolewa na UTT AMIS kwa urahisi zaidi.

(iii) Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu - UTT PID

170. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu imejiwekea malengo ya kuhakikisha inakuza mtaji kutokana na shughuli zake; Inapanua wigo wa shughuli zake ili kuwafikia wateja wengi zaidi na kuongeza mapato ya taasisi; na kuboresha miundombinu ya taasisi ili iweze kusaidia kumudu changamoto zilizopo.

4.2.7 Taasisi za Mafunzo

(i) Chuo cha Usimamizi wa Fedha – IFM

171. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Chuo cha Usimamizi wa Fedha kinatajaria kudahili wanafunzi 8000 katika fani mbali mbali. Chuo kitaendelea kuboresha shughuli zake za utafiti, kutoa machapisho na huduma kwa jamii (research, publication and consultancy). Jumla ya tafiti 9 zinategemewa kufanyika na kukamilika. Kwa upande wa huduma kwa jamii, Chuo kinatarajia kushinda kandarasi 8, pamoja na kuendesha kozi fupi na warsha zisizopungua 20 kwa mwaka 2016/17.

172. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ajira mpya na uboreshaji rasilimali watu, Chuo kinatarajia kuajiri watumishi wapya 16, watumishi 10 wanategemewa kupandishwa vyeo, na watumishi 20 wanategemewa kupata nafasi za kuendelea na masomo ya muda mrefu katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu.

173. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kitatenga fedha ambazo zitatumika katika kuliendeleza eneo lililopo katika vijiji vya Msata na Kihangaiko Wilayani Bagamoyo Mkoani Pwani kwa awamu ndogo ndogo kwa kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu. Aidha, Chuo kimeazimia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma zake kuu kwa wadau wa ndani na wa nje ya chuo. Huduma hizi ni pamoja na mafunzo kwa wanachuo kuanzia ngazi ya cheti mpaka Shahada ya Uzamili, utafiti na huduma ya utaalam shauri kwa jamii.

174. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Chuo kinategemea kuanzisha kozi tatu za Shahada za Uzamili ambazo ni "Masters of Science in Insurance and Actuarial Sciences", "Masters of Science in Social Protection, Planning and Policy" na "Masters of Science in Tax Administration".

(ii) **Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini – IRDP**

175. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kitaendelea kuboresha miundombinu katika Kampasi zake za Dodoma na Mwanza. Miundombinu hiyo itajumuisha ujenzi wa jengo la tatu la mafunzo katika kituo cha Kanda ya Ziwa jijini Mwanza na kukamilisha ujenzi wa jengo la pili la mafunzo katika Kampasi kuu Dodoma. Aidha, Chuo kinalenga kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 4622 waliodahiliwa mwaka wa masomo 2015/16 hadi kufikia wanafunzi 5000 mwaka wa masomo 2016/17. Chuo kitaendelea na mkakati wake wa kuendeleza ujuzi na uwezo kwa rasilimali watu katika viwango mbalimbali vya kitaaluma ili kuwawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa. Vilevile, Chuo kimejipanga kusaidia Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kupeleka Madaraka kwa

Wananchi kwa kuweka mkakati wa kutoa mafunzo ya Muda Mfupi ya kujenga uwezo kwa watendaji namna ya kupanga, na kusimamia mipango ya mandeleo kwenye maeneo yao ya kazi.

(iii) Taasisi ya Uhasibu Arusha – IAA

176. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2016/17 17 Taasisi ya Uhasibu Arusha kinatarajia kuwasilisha mitaala mipyä kwa ajili ya kupata ithibati kutoka NACTE. Mitaala hiyo itaainisha kozi katika ngazi ya uzamili zinazotarajiwa kutolewa na Chuo kwa kushirikiana na chuo cha TAMALE POLYTECHNIC cha nchini Ghana. Kozi hizo ni Shahada ya Uzamili ya Biashara, Stashahada ya Uzamili ya Fedha na Uwekezaji na Shahada ya Uhasibu na Ualimu.

(iv) Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA

177. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Taasisi ya Uhasibu Tanzania imepanga kukamilisha taratibu za kuanzisha kozi nne mpyä ikiwemo ile ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma katika ngazi ya cheti, diploma na shahada ili kutoa wahitimu wenyе sifa za kufanya kazi katika Serikali kuu, Serikali za Mitaa na mashirika yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Taasisi imepanga kuanza kutoa mafunzo ya shahada ya kwanza katika Kampasi ya Singida na Mwanza ili Watanzania waishio katika mikoa hiyo na ya jirani waweze kupata nafasi ya kujiendeleza kielimu. Taasisi imepanga kuendelea na uboreshaji wa miundo mbinu kwa kuendelea na ujenzi wa majengo mbali mbali katika kampasi ya Mbeya na Dar es Salaam ili kujiweka katika viwango vya taasisi za elimu ya juu.

(v) Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – EASTC

178. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016/17, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kimepanga kuendelea kutoa mafunzo ya takwimu katika ngazi ya cheti cha awali cha

takwimu rasmi, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili katika takwimu rasmi kwa watumiaji wa Chuo. Aidha, Chuo kinatarajia kutoa mafunzo ya Uzamili katika eneo la Utawala na Biashara. Mafunzo hayo yataendeshwa kwa ushirikiano na Chuo kikuu cha Nargajurna kilichopo nchini India. Vilevile, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya awali kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa takwimu wanafunzi waliomaliza elimu za Sekondari kidato cha nne.

179. **Mheshimiwa Spika**, mbali na mafunzo ya muda mrefu, Chuo kitaendelea kuwijengea uwezo wake wa ndani katika kusimamia majukumu yake. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni mafunzo kwa wakufunzi, vitendea kazi na upanuzi wa Chuo kupitia Mpango Mkakati wake. Katika kukabiliana na changamoto za ukosefu wa vyumba vyta madarasa, kumbi za mikutano na vyumba vyta maktaba, katika bajeti ya 2016/17 Chuo kimeandaa bajeti ya miundombinu ya kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa jengo la utawala, maktaba, vyumba vyta madarasa na mabweni ya wanafunzi.

180. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kitaendelea kuzisaidia Wizara, Idara za Serikali, Mashirika ya umma na Makampuni binafsi katika kujenga mifumo ya kukusanya na kuchambua takwimu kwa njia ya mtandao. Mpango huu una lengo la kuhamasisha matumizi ya takwimu sahihi zilizoandaliwa kwa wakati hivyo kuziwezesha Wizara, Idara za Serikali, Mashirika ya umma na Makampuni binafsi kusimamia vema mipango yake ya maendeleo.

4.2.8 Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo

(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA

181. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Mamlaka ya Mapato Tanzania imeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni 14,139.016 sawa na ongezeko la asilimia 14.9 ikilinganishwa na matarajio ya makusanyo ya mwaka 2015/16. Aidha, kwa upande wa

Zanzibar Mamlaka inategemea kukusanya jumla ya shilingi bilioni 209.21 sawa na ongezeko la asilimia 14.3 ikilinganishwa na matarajio ya mwaka 2015/16.

182. **Mheshimiwa Spika**, ili kudhibiti udanganyifu katika ukadiriaji, Mamlaka kwa mwaka 2016/17 imepanga kutumia njia mbalimbali zikiwemo, ushirikiano na mamlaka nyingine za mapato za nchi jirani katika kubadilishana uzoefu na kupashana habari, kuendelea kuboresha programu za ukaguzi hasa kwa kodi ambazo ukusanyaji wake unaenda kwa misingi ya ukaguzi, kama VAT, kudhibiti usimamizi wa bidhaa zinazopitia hapa nchini kwa ajili ya matumizi ya nchi jirani (*transit cargo*) hasa bidhaa za petrol na kuboresha taaluma kwa wafanyakazi.

183. **Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha mapato kwenye ushuru wa forodha na bidhaa, Mamlaka itaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:- Kutumia mfumo ulioimarishwa wa '*Import Export Commodity Database*' (IECD) kwa lengo la kuboresha na kuimarisha uthamini wa mizigo iingiayo nchini kutoka nje; Kuimarisha matumizi ya mfumo wa TANCIS kwa lengo la kuboresha makusanyo ya ushuru wa forodha; Kudhibiti usimamizi wa bidhaa zinazopitia hapa nchini kwa ajili ya matumizi ya nchi jirani (*transit*), kuboresha shughuli za ukaguzi baada ya mizigo kutoka bandarini (*Post Clearance*), na kuimarisha ukaguzi wa mizigo gatini Dar es salaam (Dar Wharf); na kuboresha usimamizi wa Mfumo wa Kieletronic wa kufuutilia Mizigo (*Electronic Cargo Tracking System*).

184. **Mheshimiwa Spika**, mikakati mingine itakayotekelawa na Mamlaka ni pamoja na kufuutilia kwa karibu ulipaji wa kodi kwa mizigo iliyokwisha kadiriwa kulipiwa kodi na waagizaji wenyewe wa mizigo hiyo na kuhakikiwa na maofisa wa Forodha lakini Malipo yake bado hayajafanywa; Kuboresha usimamiaji wa bidhaa za mafuta ya petroli zinazoingizwa nchini; Kudhibiti biashara ya magendo katika bahari ya Hindi, mipaka na njia sizizo rasmi kat i yetu na nchi za jirani; Kufanya ukaguzi wa ziada kwenye maeneo yenye viashiria vya uvujaji wa mapato, kutambua mapingamizi (*objection*) na kuyapatia ufumbuzi mapema kisheria, na kuboresha vifaa vya kufanya kazi; na

kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kusimamia kodi na kudhibiti vitendo vya rushwa kwa kupunguza umuhimu wa mlipakodi kukutana ana kwa ana na msimamizi wa kodi.

(ii) Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

185. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2016/17, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepanga kuendelea kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu rasmi zinazohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa wakati; Kufanya tafiti mbalimbali kama zilivyoainishwa katika Mpango Mkakati ili kukidhi mahitaji yaliyopo; Kuendelea kuchambua takwimu na taarifa mbalimbali zinazotokana na sensa na tafiti za kiuchumi na kijamii zinazofanywa na ofisi sambamba na uchambuzi na utoaji wa machapisho yenye takwimu mbalimbali; na kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar itaendelea na uelimishaji na uhamasishaji wa matumizi ya takwimu rasmi zinazotolewa na Ofisi hizi katika kupanga, kutunga Sera na kufanya maamuzi.

(iii) Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha – SELF Microfinance Fund

186. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2016/2017, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha unakusudia kutoa mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 13.0 huku ikijita katika kuboresha kiwango cha urejeshaji kufikia angalau asilimia 95; Kufungua ofisi ya kanda katika mikoa ya Kaskazini; na kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa asasi zipatazo 30, mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa wapao 300 na pia kwa maafisa ushirika wa mikoa 10.

(iv) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi – NBAA

187. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi imepanga kuendelea kufanya usajili wa watahiniwa, wanachama na makampuni ya uhasibu na ukaguzi; Kufanya ukaguzi na kusimamia ubora wa kazi za ukaguzi; Kutoa

miongozo ya viwango vya uhasibu na ukaguzi; Kuendeleza taaluma ya uhasibu; Kutoa mafunzo endelevu kwa wanataaluma na wadau wengine; Kusimamia mradi wa maboresha ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu; Kukamilisha ujenzi wa kituo cha wahasibu; Kusimamia uanzishaji wa mitaala mipya katika kuendesha mitihani ya Uhasibu; Kuendelea kushirikiana na mamlaka nyingine za udhibiti kama TRA, BRELA na BoT katika kuhamasisha wadau kuweza kuelewa na kutumia viwango uhasibu na ukaguzi wa hesabu vinavyokubalika.

(v) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha - Gaming Board

188. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2016/17, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha inatarajia kukusanya kodi itakayofikia shilingi bilioni 34.72, sawa na ongezeko la asilimia 26.35 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 27.48 inayotarajiwa kukusanywa katika mwaka wa 2015/16. Aidha, Bodi imejipanga kuendelea kusimamia vema sekta ya michezo ya kubahatisha nchini na kuhakikisha kwamba inaendelea kuendeshwa kwa mujibu wa sheria. Bodi inatarajia kuchangia kiasi cha Shilingi bilioni 2.17 kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina katika mwaka 2016/17 hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 50.69 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 1.44 ya mwaka wa 2015/16.

5.0 MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2016/17

5.1 MAKADIRIO YA MAPATO

189. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi **449,699,727,503** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada na mishahara isiyolipwa, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma.

5.2 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17

190. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17 kupitia mafungu yote tisa ya kibajeti inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 8,716,493,400,510 (bilioni 8,716.49)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 45,454,478,000 (bilioni 45.45)** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 8,671,038,922,510 (bilioni 8,671.04)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 791,998,424,268 (bilioni 791.99)**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 723,150,000,000 (bilioni 723.15)** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 68,848,424,268 (bilioni 68.85)** ni Fedha za Nje. Mchanganuo kwa kila fungu ni kama ifuatavyo:-

5.2.1 FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

191. ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 50,716,878,000 (bilioni 50.72)**. Kati ya hizo:
 - (i) Mishahara - **Shilingi 6,984,801,000 (bilioni 6.98)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo – **Shilingi 43,732,077,000 (bilioni 43.73)**
- (b) Miradi ya Maendeleo - **Shilingi 26,035,591,500 (bilioni 26.03)**. Kati ya hizo:
 - (i) Fedha za Ndani - **Shilingi 9,000,000,000 (bilioni 9.00)**.
 - (ii) Fedha za Nje - **Shilingi 17,035,591,500 (bilioni 17.03)**.

5.2.2 FUNGU 21 – HAZINA

192. ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 411,279,240,510 (bilioni 411.28)**. Kati ya hizo:
- (i) Mishahara ya fungu hili - **Shilingi 4,474,752,000 (bilioni 4.47)**.
 - (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 406,804,488,510 (bilioni 406.8)** ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya idara, taasisi zilizo chini ya Fungu hili, pamoja na matumizi maalum.
- (b) Miradi ya maendeleo - **Shilingi 740,155,523,400 (bilioni 740.15)**. Kati ya hizo:
- (i) Fedha za Ndani - **Shilingi 699,500,000,000 (bilioni 699.5)**
 - (ii) Fedha za Nje - **Shilingi 40,655,523,400 (bilioni 40.65)**

5.2.3 FUNGU 22- DENI LA TAIFA

193. ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 8,009,341,187,000 (bilioni 8,009.34)**. Kati ya hizo:
- (i) Mishahara - **Shilingi 9,340,716,000 (bilioni 9.34)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 8,000,000,471,000 (bilioni 8,000)**

5.2.4 FUNGU 23 – MHASIBU MKUU WA SERIKALI

194. ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

- (a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 45,585,865,000 (bilioni 45.58)**. Kati ya hizo

- (i) Mishahara - **Shilingi 6,784,116,000 (bilioni 6.78)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 38,801,749,000 (bilioni 38.8).**
- (b)** Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 4,493,750,000 (bilioni 4.49)** Kati ya hizo:
- (i) Fedha za Ndani - **Shilingi 2,000,000,000 (bilioni 2).**
 - (ii) Fedha za Nje - **Shilingi 2,493,750,000 (bilioni 2.49).**

5.2.5 FUNGU 7 – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

195. ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a)** Matumizi ya Kawaida – **Shilingi 160,181,000,000 (bilioni 160.18).** Kati ya hizo:-
- (i) Mishahara - **Shilingi 1,974,355,000 (bilioni 1.97)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 158,206,645,000 (bilioni 158.21).**
- (b)** Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 3,228,540,000 (bilioni 3.23)** Kati ya hizo:
- (i) Fedha za Ndani – **Shilingi 650,000,000 (bilioni 0.65).**
 - (ii) Fedha za Nje - **Shilingi 2,578,540,000 (bilioni 2.58).**

5.2.6 FUNGU 10 – TUME YA PAMOJA YA FEDHA

196. ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

- (a)** Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 1,374,270,000 (bilioni 1.37).** Kati ya hizo:-
- (i) Mishahara - **Shilingi 464,472,000 (bilioni 0.46)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo- **Shilingi 909,798,000 (bilioni 0.91).**

5.2.7 FUNGU 13 – KITENGO CHA UDHIBITI WA FEDHA HARAMU

197. ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kwa Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 1,603,081,000 (bilioni 1.6)**.

5.2.8 FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

198. ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a) Matumizi ya Kawaida **Shilingi 32,373,096,000 (bilioni 32.37)**. Kati ya hizo:-
 - (i) Mishahara ni **Shilingi 13,870,774,000 (bilioni 13.87)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 18,502,322,000 (bilioni 18.50)**

- (b) Miradi ya Maendeleo Fedha za Nje ni **Shilingi 12,285,427,368 (bilioni 12.28)**.
 - (i) Fedha za Ndani – **Shilingi 8,000,000,000 (bilioni 8.00)**
 - (ii) Fedha za Nje – **Shilingi 4,285,427,368 (bilioni 4.28)**

5.2.9 FUNGU 66 – TUME YA MIPANGO

199. ***Mheshimiwa Spika***, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

- (a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 4,038,783,000 (bilioni 4.04)**. Kati ya hizo:
 - (i) Mishahara - **Shilingi 1,560,492,000 (bilioni 1.56)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 2,478,291,000 (bilioni 2.48)**

- (b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 5,799,592,000 (bilioni 5.79)**. Kati ya hizo:
 - (i) Fedha za Ndani - **Shilingi 4,000,000,000 (bilioni 4)**.

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 1,799,592,000 (bilioni 1.79)**.

200. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maombi ya fedha kwa mafungu Tisa niliyoyataja katika aya ya 190 ya kitabu cha hotuba yangu, nichukue fursa hii pia kuwasilisha maombi ya fedha kwa mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) na Mfuko wa Bunge (Fungu 42). Maombi haya ni kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanyika kwenye kifungu cha 59 kifungu kidogo cha 3 cha Sheria ya Utawala wa Mahakama Sura 237 na kifungu cha 29 kifungu kidogo cha 3 cha Sheria ya Utawala wa Bunge, Sura 115, kupitia Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Sheria hizi zinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuwasilisha Bungeni maombi ya fedha za matumizi ya mifuko hii.

201. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia sheria hii, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 230,693,160,000 (bilioni 230.69)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa mafungu haya mawili. Kati ya hizo, **Shilingi 176,931,426,000 (bilioni 176.93)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 53,761,734,000 (bilioni 53.76)** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

5.2.10 FUNGU 40 – MFUKO WA MAHAKAMA

202. **Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

- (a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 84,865,309,000 (bilioni 84.86)**. Kati ya hizo:
 - (i) Mishahara - **Shilingi 50,345,775,000 (bilioni 50.35)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo – **Shilingi 34,519,534,000 (bilioni 34.52)**
- (b) Miradi ya Maendeleo - **Shilingi 46,761,734,000 (bilioni 46.76)**. Kati ya hizo:
 - (i) Fedha za Ndani - **Shilingi 24,000,000,000 (bilioni 24.00)**.

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 22,761,734,000 (bilioni 22.76).**

5.2.11 FUNGU 42 – MFUKO WA BUNGE

203. **Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

- (a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 92,066,117,000 (bilioni 92.07)**. Kati ya hizo:
 - (i) Mishahara - **Shilingi 23,798,609,000 (bilioni 23.80)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo – **Shilingi 68,267,508,000 (bilioni 68.27)**
- (b) Miradi ya Maendeleo Fedha za Ndani - **Shilingi 7,000,000,000 (bilioni 7.00)**.

5.3 SHUKRANI

204. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa ambayo kwa namna moja ama nyingine yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Finland, Uingereza kupitia shirika la DFID, Canada, Denmark kupitia shirika la DANIDA, Ireland, Japan kupitia shirika la JICA, Marekani, Norway, Sweden, Uhlanzi na Ujerumani. Pia taasisi mbalimbali za kimataifa ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Global Fund, Umoja wa Ulaya, na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNFPA na UNDP.

205. **Mheshimiwa Spika**, Napenda pia kuwashukuru sana wafanyakazi na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiari na pia kushiriki katika ujenzi wa Taifa letu. Ni imani yangu kuwa juhudini hizi zinazochukuliwa na Serikali yetu na wananchi zitatuwezesha kufikia malengo yetu ya kukuza uchumi na kupambana na umaskini.

206. ***Mheshimiwa Spika***, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.mof.go.tz).

207. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

VIAMBATISHO:

JEDWALI NA.1 TAASISI NA MASHIRIKA YALIYOCHINI YA WIZARA

NA:	TAASISI/ SHIRIKA	MAJUKUMU
1	Ofisi ya Msajili wa Hazina - TRO	Usimamizi wa Rasilimali za Serikali.
2	Benki Kuu ya Tanzania - BOT	Kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kudhibiti mfumko wa bei na hivyo kuweka mazingira bora ya kukuza uchumi, mazingira ya kifedha ambayo yataleta kiwango cha chini cha mfumuko wa bei kisichobadilika mara kwa mara na kinachokaribiana na wastani wa viwngo vya mfumuko wa bei katika nchi zinazofanya biashara na Tanzania.
3	Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA	Kukusanya mapato yatokanayo na Kodi.
4	Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma – PSPF	<ol style="list-style-type: none"> 1. Kusajili wanachama na waaajiri kwenye mfuko; 2. Kukusanya michango ya wanachama kutoka kwa waajiri; 3. Kulipa mafao na stahili zingine kwa wanachama wanaostahili; 4. Kufanya uwekezaji wa ziada inayopatikana kwenye miradi inayolipa; na kutoa taarifa ya fedha za wanachama.
5	Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali - GEPF	<ol style="list-style-type: none"> 1. Kusajili wanachama na waaajiri kwenye mfuko; 2. Kukusanya michango ya wanachama kutoka kwa waajiri; 3. Kulipa mafao na stahili zingine kwa wanachama wanaostahili; 4. Kufanya uwekezaji wa ziada inayopatikana kwenye miradi inayolipa; na kutoa taarifa ya fedha za wanachama.

NA:	TAASISI/ SHIRIKA	MAJUKUMU
6	Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma - PPRA	<p>1. Kuishauri serikali kuhusu masuala ya manunuizi;</p> <p>2. Kusimamia uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake;</p> <p>3. Kuandaa nyaraka za zabuni kwa jaili ya shughuli za ununuzi;</p> <p>4. Kuweka mikakati ya kujenga uwezo katika taaluma ya manunuizi; na;</p> <p>5. Kuwezesha kupatikana muafaka katika migogoro ya manunuizi</p>
7	Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima - TIRA	Kusimamia na kuthibiti shughuli za Bima nchini.
8	Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma - PPF	<p>1. Kusajili wanachama na waajiri kwenye mfuko;</p> <p>2. Kukusanya michango ya wanachama na kutoka kwa waajiri;</p> <p>3. Kulipa mafao na stahili zingine kwa wanachama wanaostahili; na</p> <p>4. Kufanya uwekezaji kwenye miradi mbalimbali.</p>
9	Taasisi ya Uhasibu Tanzania - TIA	<p>1. Kutoa elimu bora katika michepuo ya uhasibu, ununuzi na michepuo mingine ya kibia shara na</p> <p>2. Kufanya tafiti na kutoa ushauri katika maswala ya uhasibu na ununuzi kwenye sekta ya umma na binafsi.</p>
10	Chuo cha Usimamizi wa Fedha - IFM	Kufundisha, kutoa huduma ya ushauri elekezi na kufanya utafiti.
11	Chuo cha Uhasibu Arusha - IAA	Kutoa elimu katika michepuo ya uhasibu, ununuzi na michepuo mingine ya biashara na huduma ya ushauri elekezo katika masuala ya uhasibu na ununuzi kwenye sekta ya umma na binafsi.

NA:	TAASISI/ SHIRIKA	MAJUKUMU
12	Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki – EASTC	Kufundisha, kufanya utafiti nakutoa ushauri kuhusu maswala mbalimbali ya kitakwimu.
13	Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - IRDP	Kutoa mafunzo na utafiti wa mipango ya maendeleo vijijini ili kuweza kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kiushauri Serikali katika kuandaa sera za mipango ya maendeleo vijijini.
14	Kitengo cha Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu - FIU	Kuhakikisha kuwa mfumo wa fedha wa Tanzania hauathiriwi na biashara ya fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi kwa kupokea taarifa zenyenye mashaka juu ya biashara ya fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi kutoka kwa watoa taarifa, kuzifanyia uchambuzi na kisha kuwasilisha matokeo ya uchambuzi kwa vyombo vyaya kusimamia sheria kwa ajili ya uchunguzi na hatua zaidi za kisheria.
15	Ofisi ya Taifa ya Takwimu - NBS	Kutoa huduma za kitakwimu nchini.
16	Mamlaka ya Rufaa za Zabuni - PPAA	Kushughulikia rufani za wazabuni.
17	Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini - GPSA	Kufanya ununuzi kwa niaba ya Wizara, Idara na wakala za Serikali.
18	Tume ya Pamoja ya Fedha - JFC	Kuishauri Serikali katika masuala ya fedha za Jamhuri ya Muungano yanayohusu matumizi ya kawaida katika serikali zote mbili.
19	Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu - UTT-PID	Uanzishwaji, utekelezaji na usimamiaji wa miradi mikubwa yenye umuhimu kiuchumi na kijamii na kutoa huduma ya kusimamia na kutunza majengo (Property management).
20	Taasisi ya Huduma za fedha na Mikopo - UTT-MFI	Kutoa huduma shirikishi za kifedha na mikopo midogo midogo kwa mwananchi mmoja mmoja, SACCOS, Vikundi nk. Kutoa huduma za kifedha kuitia ;miamala ya

NA:	TAASISI/ SHIRIKA	MAJUKUMU
		mitandao na wavuti na kupokea amana, Hati fungani n.k.
21	Taasisi ya Huduma za Uwekezaji wa Pamoja - UTT-AMIS	<p>1. Kuanzisha na kusimamia mifuko ya uwekezaji wa pamoja.</p> <p>2. Kutoa huduma za ushauri wa masuala ya uwekezaji na kutoa huduma za usimamizi wa mitaji</p>
22	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha - GBT	Kusimamia michezo wa kubahatisha
23	Benki ya Maendeleo ya TIB -TIB DFI	<p>1. Kutoa mikopo ya muda wa kati na mrefu kwa wawekezaji katika sekta mbalimbali.</p> <p>2. Benki mama ya TIB Corporate Bank.</p>
24	Benki ya Biashara TIB –TIB CFL	Kutoa mikopo ya muda mfupi pamoja na huduma za kibenki za biashara kwa benki ya maendeleo ya TIB na Benki ya Kilimo (TADB), pamoja na wateja wengine.
25	Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB	Madhumuni ya kusaidia upatikanaji utoshelezi na usalama wa chakula endelevu nchini na kusaidia katika kuleta mapinduzi ya kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kilimo cha biashara ili kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.
26	Mamlaka ya Masoko ya Mitaji ya Dhamana - CMSA	<p>1. Kuhamasisha na kuendeleza masoko ya mitaji Tanzania na kweka mazingira yaliyo sawa katika biashara ya mitaji na dhamana;</p> <p>2. Kuweka sheria na kanuni za kuwalinda wawekezaji;</p> <p>3. Kuishauri Serikali katika masuala ya mitaji na dhamana; na</p> <p>4. Kutoa idhini, kusimamia na kutoa leseni kwa masoko ya mitaji, mawakala na waendeshaji wengine katika soko la mitaji.</p>
27	Mfuko wa Huduma za	Kukuza na kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha

NA:	TAASISI/ SHIRIKA	MAJUKUMU
	Fedha (SELF Microfinance Fund)	kwa wananchi wa vijiji na mijini.
28	Bodi ya Wataalamu Ununuzi na Ugavi - PSPTB	Kusimamia na kudhibiti taaluma ya ununuzi na ugavi.
29	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Ukagazi - NBAA	Kusimamia taaluma ya uhasibu na ukagazi.
30	Benki ya Posta Tanzania - TPB	<ol style="list-style-type: none"> 1. Kukusanya amana za wateja na kujenga miongoni mwao tabia ya kujiwekea akiba 2. Kutoa huduma bora za kibenki katika Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Sheria za Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991. 3. Kukusanya rasilimali za hapa nchini kwa kupokea amana kutoka kwa wateja. 4. Kusimamia mifuko maalum kwa niaba ya Serikali itakayowekwa mikononi mwa benki hii kwa mujibu wa sheria iliyoienda. 5. Kuendesha shughuli zote zinazoendeshwa na mabenki ya biashara, ikiwemo utoaji mikopo kwa wananchi na shughuli za fedha za kigeni.
31	Benki ya Twiga - Twiga Bancorp LTD	Kuhifadhi fedha za wateja nakutoa mikopo na huduma nyingine za kibenki.
32	Shirika la Bima la Taifa - NIC	Kukusanya tozo za wanachama; na kulipa madeni ya wanachama kutokana na bima zao pale inapohitajika.
33	Baraza la Rufani za Kodi - TRAT	Kupokea, kusikiliza na kutolea uamuzi wa migogoro yote ya kodi itokanayo na uamuzi wa Bodi ya Rufani za Kodi.
34	Bodi ya Rufani za Kodi - TRAB	Kuamua kwa haraka migogoro yote ya kodi inayotokea baina ya walipa kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania.
35	Soko la Hisa la Dar es	Kuwezesha Serikali katika utekelezaji wa Sera za Uchumi

NA:	TAASISI/ SHIRIKA	MAJUKUMU
	Salaam - DSE	katika Sekta ndogo ya Fedha.

JEDWALI NA.2 : Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida Mwaka 2015/16

FUNGU	FEDHA ZILIZO IDHINISHWA 2015/16	MATUMIZI HADI MACHI, 2016	ASILIMIA
FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO			
Mishahara	7,624,713,642	4,584,508,000	60
Matumizi Mengineyo	55,430,333,191	28,404,958,991	51
Jumla Fungu 50	63,055,046,834	32,989,466,991	
FUNGU 23 – IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI			
Mishahara	7,932,329,000	4,784,723,500	60
Matumizi Mengineyo	103,680,371,937	63,690,690,294	61
Jumla Fungu 23	111,612,700,937	68,475,413,794	
FUNGU 22 – DENI LA TAIFA			
Mishahara	9,030,000,000	4,712,737,442	52
Matumizi Mengineyo	6,381,430,000,000	3,953,237,899,024	62
Jumla Fungu 22	6,390,460,000,000	3,957,950,636,467	
FUNGU 21 - HAZINA			
Mishahara	4,960,000,000	2,740,508,400	55
Matumizi Mengineyo	650,460,000,000	495,023,583,050	76
Jumla Fungu 21	655,420,000,000	497,764,091,450	
FUNGU 13 – KITENGO CHA KUDHIBITI FEDHA HARAMU			
Mishahara	0	0	0
Matumizi Mengineyo	930,000,000	414,864,718	45
Jumla Fungu 13	930,000,000	414,864,718	
FUNGU 10 – TUME YA PAMOJA YA FEDHA			

Mishahara	904,792,000	341,924,000	38
Matumizi Mengineyo	928,465,000	316,511,651	34
Jumla Fungu 10	1,833,257,000	658,435,651	
FUNGU 7 – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA			
Mishahara	2,649,137,000	1,381,008,832	41
Matumizi Mengineyo	22,399,881,000	11,233,764,941	50
Jumla Fungu 7	25,049,018,000	12,614,773,775	
FUNGU 66 – TUME YA MIPANGO			
Mishahara	2,500,007,000	1,070,485,990	43
Matumizi Mengineyo	3,249,799,000	1,156,386,750	36
Jumla Fungu 66	5,749,806,000	2,226,872,740	
FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI			
Mishahara	14,209,821,000	10,059,558,216	71
Matumizi Mengineyo	49,304,829,000	29,608,736,000	60
Jumla Fungu 45	63,514,650,000	39,668,294,216	
JUMLA KUU	7,317,624,478,770	4,612,762,849,799	

JEDWALI NA. 3: Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha za Maendeleo 2015/16

FUNGU	Fedha zilizoidhinishwa mwaka 2015/16	Matumizi hadi Machi, 2016	% ya Matumizi
FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO			
Fedha za Ndani	7,255,300,000	0	0
Fedha za Nje	358,544,428,000	5,527,212,244	1.5
Jumla Fungu 50	365,799,728,000	5,527,212,244	
FUNGU 23 – IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI			
Fedha za Ndani	2,000,000,000	2,000,000,000	100
Fedha za Nje	1,673,845,000	718,940,000	43
Jumla Fungu 23	3,673,845,000	2,718,940,000	
FUNGU 21 - HAZINA			
Fedha za Ndani	638,731,900,000	0	0
Fedha za Nje	9,034,366,000	10,177,557,111	112
Jumla Fungu 21	647,766,266,000	10,177,557,111	
FUNGU 13 – KITENGO CHA KUDHIBITI FEDHA HARAMU			
Fedha za Ndani	0	0	0
Fedha za Nje	35,768,000	0	0
Jumla Fungu 13	35,768,000	0	0
FUNGU 7 – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA			
Fedha za Ndani	650,000,000	0	0
Fedha za Nje	349,885,000	0	0
Jumla Fungu 7	999,885,000	0	0

FUNGU 66 – TUME YA MIPANGO			
Fedha za Ndani	2,000,000,000	678,200,000	34
Fedha za Nje	816,156,000	451,282,000	55
Jumla Fungu 66	2,816,156,000	1,129,482,000	
FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI			
Fedha za Ndani	8,000,000,000	0	0
Fedha za Nje	2,667,116,000	2,253,306,965	84
Jumla Fungu 45	10,667,116,000	2,253,306,965	
JUMLA KUU	1,031,758,764,000	21,806,498,320	

**JEDWALI NA.4: Malengo na Makusanyo Halisi Katika Kipindi cha Mwezi Julai,
2015 – Machi, 2016 cha mwaka 2015/16**

(Shilingi bilioni)

Idara	2014/15 (Julai – Machi, 2016)	2015/16 (Julai – Machi, 2016)		Ufanisi (%)	% ya Ukuaji
	Makusanyo Halisi	Lengo	Makusanyo Halisi		
Kodi za Ndani	1,451.19	1,709.83	1,785.71	104	23
Walipakodi Wakubwa	3,432.95	4,182.84	4,050.67	96.8	17.99
Ushuru wa Forodha	3,057.25	3,963.55	3,928.55	99.1	28.5
Jumla 1	7,941.39	9,856.22	9,764.94	99.1	22.96
Jumlisha: Hati za Serikali.	13.64	24.31	16.57	68.0	21.16
Jumla 2	7,955.03	9,880.53	9,781.47	99.0	22.96
Toa: Marejesho na Uhawilisho	556.4	645.54	529.59	82.0	-4.82
Jumla 3 (Net Collections)	7,398.6	9,234.99	9,251.87	100.2	25.00

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania

**JEDWALI NA. 5: Malengo na Makusanyo Halisi Katika Kipindi cha Mwezi Julai –
Februari, 2016 cha mwaka 2015/16 (TRA Zanzibar)**

(Shilingi bilioni)

Idara	2014/15	2015/16			% ya Ukuaji
	Makusanyo Halisi	Lengo	Makusanyo Halisi	Ufanisi (%)	
Kodi za Ndani	41.10	47.18	48.61	103.02	18.3
Ushuru wa Forodha	65.75	85.10	72.45	85.17	10.2
Jumla	106.85	132.28	121.06	91.54	13.31

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania